BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KIDATO CHA SITA, 2018

121 KISWAHILI

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE) 2018

121 KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2018**

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI iv
1.0 UTANGULIZI 1
2.0 SEHEMU YA 1: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA 2
2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI 2
2.2 SEHEMU A: UFAHAMU 2
2.2.1 Swali la 1: Ufahamu 2
2.2.2 Swali la 2: Ufupisho 8
2.3 SEHEMU B: MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA .. 11
2.3.1 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi 11
2.3.2 Swali la 4: Matumizi ya Sarufi 16
2.3.3 Swali la 5:Utumizi wa Lugha 21
2.3.4 Swali la 6: Utumizi wa Lugha 26
2.4 SEHEMU C: UTUNGAJI 29
2.4.1 Swali la 7: Utungaji 29
2.5 SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI 32
2.5.1 Swali la 8: Ukuaji wa Lugha ya Kiswahili. 32
2.5.2 Swali la 9: Maendeleo ya Kiswahili 40
2.6 SEHEMU E: TAFSIRI NA UKALIMANI 47
2.6.1 Swali la 10: Tafsiri 47
3.0 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI 53
3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI 53
3.2 SEHEMU A: FASIHI KWA UJUMLA 53
3.2.1 Swali la 1: Fasihi kwa Ujumla 53
3.2.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla 59
3.3 SEHEMU B: USHAIRI 66
3.3.1 Swali la 3: Uhakiki wa Ushairi 66
3.3.2 Swali la 4: Uhakiki wa Ushairi 74
3.4 SEHEMU C: RIWAYA 83
3.4.1 Swali la 5: Uhakiki wa Riwaya 83
3.4.2 Swali la 6: Uhakiki wa Riwaya. 89
3.5 SEHEMU D: TAMTHILIYA 97
3.5.1 Swali la 7: Uhakiki wa Tamthiliya 97
3.5.2 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya 104
3.6 SEHEMU E: USANIFU WA MAANDISHI 111
3.6.1 Swali la 9: Usanifu wa Maandishi 111
4.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA 115
5.0 HITIMISHO 116
6.0 MAONI NA MAPENDEKEZO 116
Kiambatisho A 118
Kiambatisho B 119

DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa kuhusu uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Kidato cha Sita mwaka 2018 katika somo la Kiswahili ili kutoa mrejesho wa kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho yenye lengo la kuonesha ni jinsi gani mfumo wa elimu nchini umefanikiwa kutoa elimu kwa ujumla hususani katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Aidha, majibu ya watahiniwa katika mtihani huu yanalenga kuonesha maarifa ambayo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa kwa elimu ya juu ya Sekondari.

Taarifa hii imechambua sababu mbalimbali zilizochangia watahiniwa kujibu vizuri, wastani au vibaya maswali ya mtihani huu. Matokeo ya taarifa hii yamebainisha baadhi ya sababu zilizochangia watahiniwa wengi kufanya vizuri au kwa kiwango cha wastani na kwa wachache waliokuwa na kiwango hafifu cha kufaulu. Sababu za baadhi ya watahiniwa kutojibu maswali kwa usahihi ni pamoja na kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali katika somo na kukosa maarifa kuhusu kanuni na matumizi ya lugha kwa ujumla. Aidha, uchambuzi huu umeonesha pia sababu za watahiniwa kujibu maswali kwa usahihi kama vile kutambua matakwa ya swali, kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa na kuzingatia kanuni na matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Pia, sababu za watahiniwa kupata alama za wastani zimebainishwa haswa katika kutoa majibu yasiyojitosheleza. Sababu hizi na nyinginezo zilizoainishwa katika taarifa hii zitawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu muafaka katika kuboresha kiwango cha kufaulu katika mitihani ijayo inayotolewa/inayooendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania liko tayari kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na umma kwa ujumla ambayo yatatumika katika kuboresha taarifa za uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika siku za usoni.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru maafisa mitihani, walimu wa somo na wengine wote waliohusika katika kuandaa ripoti hii. Shukrani za pekee pia ni kwa wafanyakazi wa Idara ya Utafiti, Tathmini na Huduma za Kompyuta walioshiriki katika uchambuzi wa data zilizotumika katika taarifa hii.

Dr. Charles E. Msonde
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii ni uchambuzi wa viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Kidato cha Sita mwaka 2018 kwa somo la **121 Kiswahili** uliofanyika Mei, 2018. Mtihani huu ulizingatia Muhtasari wa mwaka 2009 kwa somo la Kiswahili Kidato cha V na VI. Mtihani huu ulikuwa na karatasi mbili (2) yaani **121/1 Kiswahili 1** na **121/2 Kiswahili 2**.

Mtihani wa **121/1 Kiswahili 1** uligawanyika katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za *Ufahamu*, *Utumizi wa Lugha*, *Matumizi ya Sarufi*, *Utungaji*, *Maendeleo ya Kiswahili* na *Tafsiri na Ukalimani*, ambapo kila sehemu ilikuwa na alama (20). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali saba (7) kati ya maswali kumi (10) yaani; Sehemu A na B maswali mawili (2) kwa kila sehemu; na sehemu C, D na E, swali moja kwa kila sehemu.

Mtihani wa **121/2 Kiswahili 2** uligawanyika katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za *Fasihi kwa Ujumla, Ushairi, Riwaya, Tamthiliya na Usanifu wa Maandishi* na kila sehemu ilikuwa na alama (20) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matano (5) kwa kuchagua swali moja kutoka katika kila sehemu.

Idadi ya watahiniwa waliofanya Mtihani wa 121 Kiswahili kwa mwaka 2018 walikuwa **20,420** ambapo wanaume ni **10,362** na wanawake ni **10,058**. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani kilikuwa kizuri ambapo asilimia **99.97** ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata wastani wa alama 35 na zaidi. Viwango vya kufaulu vimegawanyika katika sehemu kuu tatu yaani; "vizuri," "wastani" na "hafifu." Kiwango kizuri cha kufaulu kinaanzia alama 60 hadi 100; kiwango cha wastani kuanzia alama 35 hadi 59 na kiwango hafifu cha kufaulu ni kuanzia alama 0 hadi 34. Aidha, chati na majedwali ya viwango vya kufaulu yameambatanishwa ili kufafanua kiwango anuai cha kufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha kiwango kizuri, rangi ya njano kuwakilisha kiwango cha wastani na rangi nyekundu kuwakilisha kiwango hafifu cha kufaulu.

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu ili kukuza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Aidha, sampuli za majibu ya watahiniwa kwa kila swali zimewekwa kwa lengo la kuonesha kilichofanywa na watahiniwa. Pia, sababu zilizowafanya watahiniwa kupata alama za juu, wastani na hafifu zimejadiliwa, ili kuweka mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa mada ambazo hazikufanya vizuri katika mtihani huu.

2.0 SEHEMU YA 1: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI

2.2 SEHEMU A: UFAHAMU

2.2.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lililenga kupima ufahamu. Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma kwa makini kifungu cha habari na kisha, kujibu kwa usahihi maswali yanayofuata. Maswali hayo yaligawanyika katika vipengele (a) hadi (d) ambavyo vilikuwa na jumla ya alama 10.

Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha habari aliyoisoma kisichozidi maneno matatu, na kilikuwa na alama 1.

Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kutoa maana ya maneno kama yalivyotumika katika habari aliyoisoma na kilikuwa na vipengele vidogo vitano (5) na kila kipengele kilikuwa na alama 1.

Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa kutoa maana ya usemi usemao, "Mungu hamtupi mja wake" kama ulivyotumika katika kifungu cha habari aliyoisoma. Kipengele hiki kilikuwa na alama 2.

Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa aeleze mchango wa wakoloni wa kiingereza katika kukuza na kueneza Kiswahili na kilikuwa na alama 2 .

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (20,418) waliofanya mtihani na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na idadi kubwa ya watahiniwa. Asilimia 93.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani na zaidi kutokana na kujibu vipengele vingi vya ufahamu kwa usahihi. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.



Chati Na. 1: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 59.9 ya watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Hii inaonesha watahiniwa walikielewa vyema kifungu cha habari na kuweza kujibu vipengele vingi kwa usahihi. Miongoni mwao, asilimia 17.4 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10 kwa kuweza kuandika kwa usahihi kichwa cha habari, kutoa maana za maneno kama yalivyotumika katika habari, kutoa ufafanuzi mzuri wa kauli isemayo "Mungu hamtupi mja wake" kama ilivyotumika katika habari waliyoisoma na kuelezea mchango wa wakoloni wa kiingereza katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu katika swali hili kwa kujibu kwa usahihi vipengele (a), (b) na (d) na kutoa ufafanuzi usiojitosheleza katika kipengele (c) pekee.

Kielelezo 1.1



01. a) USANIFISHAJI WA KISWAHILI

b) i) Usanifishaji
Ni kitendo cha kuilinganisha lugha na kuifanya ikubalike miongoni mwa watumiaji wake

ii) Zilipamba moto
Neno hili lina maana kuwa zilishamiri

iii) Lahaja
Ni tofauti ndogondogo zinazojitokeza kwenye lugha kuu yenye asili moja. Tofauti hizo hujitokeza kwenye matamshi, misamiati, maumbo na mvundo ya maneno.

iv) Kiswahili sanifu.
Ni kiswahili ambacho ni sahihi na kinachokubalika katika matumizi yake katika jamii.

v) Sudi
Neno hili lina maana ya bahati

c) Usemi huu unamaanisha kuwa Mungu hamuachi yole anayemlegemea na anayestahili. Hiyo ndiyo sababu lahaja ya kiunguja ilileuliwa kusani ilikuwa inastahili kuwa msingi wa kiswahili sanifu.

01 (d) Mwandishi anaonesha kuwa utawala wa wakoloni wa kiingereza ndio uliosaisia kukuza na kueneza lugha ya kiswahili kupitia mchakato mzima wa usanifishaji vilevile kupitia sera na mfumo wa utawala wa wakati huo ulifanya kazi ya kueneza na kukuza lugha ya kiswahili.

Kielelezo 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika kichwa cha habari kwa usahihi, kueleza maana ya misamiati iliyotumika katika habari na kueleza mchango wa waingereza katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili kama ilivyotakiwa.

Watahiniwa wengine asilimia 33.9 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali kwa baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kujibu kipengele (c) alitoa maana ya jumla ya usemi "Mungu hamtupi mja wake" bila kuhusisha maana iliyo katika kifungu cha habari na kupata alama za wastani. Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyojitosheleza katika vipengele (a), (b) (i), (iii), (v) na (c).

Kielelezo 1.2

1a) USANIFISHAJI WA KISWAHILI

b) i) Usanifishaji ÷ Ni hali ya kufanya lugha itumike kwa namna moja kwa watumiaji wake wote.

ii) Zilipamba moto ÷ kushika hatamu na kuzidi kusonga mbele katika kufanya jambo hasika.

iii) Lahaja ÷ Ni vilugha vidogo vidogo ndani au katika lugha kuu moja.

iv) Kiswahili Sanifu ÷ Ni Kiswahili ambacho kinafuata misingi yote ya lugha kimaana, kimatamshi, mantiki na kimaumbo.

v) Sudi ÷ Bahati / Ni hali ya kutunukiwa kupata nafasi ya kuwa mstari wa mbele au wa kwanza.

c) Mungu hamtupi mja wake ÷
Maana yake ni kwa Mungu hana upendeleo na akiamua kukutendea mijiza hakuna anayeweza kupinga wala kwenda kinyume na hilo



1.d) i) Kupitia Sera na mfumo wa Utawala wao walifanya kazi na Kuhakikisha Kiswahili kinakua na kuenea katika nchi za Afrika Mashariki.

ii) Kushughulikia suala zima katika - Usanifishaji wa lahaja ya Kiunguja

iii) Kuhakikisha kwamba kamati ya lugha ya Afrika Mashariki inafanya kazi yake kwa usahihi, kama kusahihisha lugha katika vitabu.

Kielelezo 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele.

Aidha, watahiniwa wachache, asilimia 6.2 walipata alama kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kutokielewa kifungu cha habari na hivyo kushindwa kujibu vipengele vingi vya maswali yaliyoulizwa. Baadhi yao, waliandika kichwa cha habari chenye maneno matano na zaidi badala ya maneno matatu na wengine walitoa maana ya neno 'sudi' kama jina la mtu badala ya bahati njema/nzuri kama ilivyotumika katika kifungu cha habari. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kujibu kipengele (a) aliandika kichwa cha habari kuwa ni "AFRIKA" badala ya USANIFISHAJI WA KISWAHILI, katika kipengele (b) alishindwa kutoa maana sahihi ya maneno (ii) *Zilipamba moto*, (iii) *lahaja* na (iv) *Kiswahili sanifu* kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Katika kipengele (c) alielezea usemi "Mungu hamtupi mja wake" kwa kutoa maelezo yasiyokidhi matakwa ya swali kwa kuandika; *Mungu hasahau yote yaliyofanyika*, kinyume na maana halisi kutoka katika kifungu cha habari. Kielelezo 1.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini kwa kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali katika vipengele vingi.

Kielelezo 1.3

1. (a) AFRIKA.

(b) (i) Usanifishaji, Ni ~~namna~~ njia iliyo tumika kuunda kamati ya Lugha ya kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki.

(ii) Zilipamba moto, Ina maana kwamba nchi za Afrika Mashariki zilifanya juu chini kutafiti lahaja za kiswahili.

(iii) Lahaja, Ni vilugha vilivyoundwa katika vipengele mbalimbali ambavyo vinatumia maneno yanayofanana.

(iv) kiswahili sanifu, Ni lugha iliyoch aguliwa kutumika katika nchi za Afrika mashariki

1. (b) (v). Sudi, Ina maana kwamba ~~lahaji~~ tafiti iliangukia kwa lahaja ya kiunguja na kuchaguliwa kuwa kuwa lahaja ya kiswahili sanifu.

c, Mungu hasahau yote yanayofanyika.

d) Mchango ambao wakoloni walichan gia kukuza na kueneza lugha ya kiswahili ni kupitia sera na mfumo wa utawala wa wakati huo. wali fanya kazi kubwa kuhakikisha kuwa kiswahili kinakuwa na kuenea katika nchi za Afrika Mashariki

Kielelezo 1.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vipengele vingi vya ufahamu kutokana na uelewa mdogo wa kifungu cha habari. Hata hivyo, mtahiniwa huyo aliweza kutoa majibu sahihi katika kipengele (d) pekee na kupata alama za chini.

2.2.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Ufupisho* na lililenga kupima uundaji. Swali lilimtaka mtahiniwa kufupisha habari aliyoisoma kwa maneno mia moja (100) na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyofanywa vizuri na watahiniwa wengi. Asilimia 93.0 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.



Chati Na 2: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 57.1 ya watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Kati yao, asilimia 9.5 walipata alama za juu kuanzia alama 8 hadi 10 kwani waliweza kuzingatia taratibu zote za ufupisho ambazo ni; *kufupisha habari kwa kutumia maneno yao wenyewe bila kupotosha kiini cha habari waliyopewa, mtiririko mzuri wa mawazo yenye mantiki wenye kuzingatia taratibu za uandishi, matumizi ya lugha sanifu na kuzingatia idadi ya maneno.* Kielelezo 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika ufupisho kwa kuzingatia taratibu zote za kufupisha habari.

Kielelezo 2.1



2. - Ufupisho wa habari;

Mwaka 1930 hadi 1938 ni mwaka ambao Usanifishaji wa lugha ya kiswahili ulianza ku Shamiri Kamati iliundwa kwa lengo la kukuza na kuendeleza lugha Afrika Mashariki.

Kamati ya lugha ililenga kufanya usawazishaji wa maandishi yote, kuandaa kamusi pamoja na kutoa hamasa kwa waandishi Mlachanga wa vitabu vinavyotumika shuleni.

Kamati hii ilikuwa chini ya utawala wa Mwingereza ambapo tafiti nyingi zilifanywa kuhusu lahaja ambazo zilizua kiswahili sanifu.

Kiunguja kiliteuliwa na kuwa lahaja ya usanifishaji na kuleta wivu kwa lahaja nyingine ambazo hazikuchaguliwa.

Utawala wa mwingereza ndio uliskuza na kuendeleza lugha ya kiswahili katika sen yake ya utawala kuliko wakoloni wengine wote.

Kielelezo 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefupisha habari kwa usahihi kwa maneno yake mwenyewe bila kupotosha kiini cha habari, mtiririko mzuri wa mawazo, kuzingatia taratibu za uandishi na idadi ya maneno ilivyotakiwa.

Asilimia 35.9 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kuandika ufupisho wenye mapungufu kama vile *kuzidisha idadi ya maneno*, *kutokuwa na mtiririko mzuri wa mawazo wenye mantiki*, *kutozingatia taratibu za uandishi ipasavyo na kutumia baadhi ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari*. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika ufupisho kwa kuzingatia baadhi tu ya vipengele muhimu katika kufupisha habari.

Kielelezo 2.2



Kielelezo 2.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kuandika ufupisho usiozingatia idadi ya maneno.

Aidha, asilimia 7.0 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 na kati yao, asilimia 0.2 walipata alama 0 kutokana na kutoelewa kabisa taratibu za kufupisha kifungu cha habari. Katika majibu yao baadhi, walinakili kifungu chote cha habari na wengine walifupisha habari kwa maneno zaidi ya mia moja (100). Kielelezo 2.3 ni majibu ya mtahiniwa aliyefupisha habari kwa kutumia maudhui yasiyolingana na kifungu cha habari alichopewa kwa kuelezea asili/chimbuko la Kiswahili badala ya kujikita katika usanifishaji wa Kiswahili na kupata alama 0.

Kielelezo 2.3



2. Kiswahili kina historia pana katika kuwa kwake, kwani zipo nadharia mbalimbali za lugha ya kiswahili zinazodai kuwa lugha hiyo adhimu ya kiswahili asili yake ni ipi, nadharia hizo zina uhahidi na nyingine zimekosa uthibitisho wa asili hizo.

Wapo wanazidai kiswahili ni Kikongo kwani wanasema kiswahili kilianzia Congo kutokana na sababu za ~~vita~~ kivita, ukame walihama kwingia Tanganyika (Tanzania) kupitia Tanduma na Ikagera, dai hili si la kweli kwani halina uthibitisho kwa walihama zini na wakingia zini Tanzania.

Pia wengine wanasema kiswahili ni Kiarabu, Krioli, Kipijini Takini nadharia hizi

Kielelezo 2.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefupisha habari kwa kubadili kiini cha habari aliyopewa kwa kuelezea nadharia za asili/chimbuko la Kiswahili kama vile *Kiarabu, Pijini,* na *Krioli* kinyume na matakwa ya swali.

2.3 SEHEMU B: MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

2.3.1 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* na lililenga kupima maarifa. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua vipengele vifuatavyo: (a) Ngeli za majina, (b) Mofimu, (c) Kirai, (d) Sentensi na (e) Mzizi. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali lilikuwa la kuchagua na asilimia 95.2 ya watahiniwa walijibu swali hili. Swali hili lilijibiwa vizuri ambapo asilimia 89.7 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na 1. linaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.

Jedwali Na. 1: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Watahiniwa	Asilimia ya Watahiniwa
0.0 - 3.0	2,006	10.3
3.5 - 5.5	6,495	33.4
6.0 - 10.0	10,939	56.3

Asilimia 56.3 ya watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10 na miongoni mwao, asilimia 20.3 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana za kisarufi walizopewa. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua vipengele vyote vitano kwa usahihi na kupata alama za juu.

Kielelezo 3.1



3. a) Ngeli za majina.

Ni mfumo wa upangaji wa nomino mbalimbali zinazofanana katika kundi moja. La nomino hizo. Katika lugha ya kiswahili Ngeli za majina zimecinishwa kwa kutumia mitazamo miwili ambago ni

i) Mtazomo wa kimapokeo, unaohusisha upangaji wa nomino kwa kuzingatia maumbo ya nomino katika umoja na wingi. Ambapo kutokana na upangaji hao zinapatikana ngeli za nomino 18.

ii) Mtazamo wa kisasa, uncohusisha upangaji wa nomino kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. Upatanisho wa kisarufi ni uhusiano uliopo katika ya nomino, kivumishi na kitenzi. Kutokana na mtazamo huu tunapata ngeli 9 za nomino.

Mwisho ngeli za nomino pia husaidia katika kathibitisha ubantu wa kiswahili pamoja na upatanisho wa kisarufi katika lugha.

b) Mofimu.

Ni kipashio kidogo kabisa katika lugha chenye maana katika sarufi na kileksika.

Katika mofimu kuna aina kuu mbili ambazo ni;

i) Mofimu huru, ambazo huvimama peke yake na kujitegemea kama neno huru. na mfano ni mofimu huru Baba, Mama, na Mjomba.

ii) Mofimu tegemezi, hizi ni mofimu ambazo haziwezi kuvimama na kujitegemea peke yake kama neno huru hadi zifungamanishwe na mofimu nginginezo. Mfano Analima.

A-na-lim-a.

3. b) Mofimu zina chhima zifuatazo.
i) Kuonesha nafsi
ii) Kuonesha wakati
iii) Kuonesha [illegible]
iv) Kuonesha urejeshi

c) Kirai.
Ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja na kuendelea ambacho hakina muundo wa kiima na kiarifu. Kirai kina sifa zifuatazo:-
i) Kirai ni tungo
ii) Kirai ni kikubwa kuliko neno na kidogo kuliko kishazi
iii) Kirai hutokea upande wa kiima na pia kiarifu.
Pia kuna miundo mbalimbali ya kirai kama vile
i) Kirai nomino
ii) Kirai kitenzi
iii) Kirai kielezi
iv) Kirai kivumishi
v) Kirai kiunganishi.

d) Sentensi
Ni tungo yenye kiima na kiarifu inayotoa ujumbe kamili. Katika lugha sentensi ni kipashio kikubwa kuliko vyote. Sentensi hutumika hutoa ujumbe pamoja na kukamilisha (kuundu aya. Pia kuna aina za sentensi kama zifuatazo
i) Sentensi sahiri
ii) Sentensi ambatano

3. d) iii) Sentensi changamano
iv) Sentensi shurutia.

e) Mzizi
Ni sehemu ya neno inayobaki baada ya kuondolewa kwa viambishi awali vyote pamoja na tamati. Au ni sehemu na neno isiyobadilika.
Katika lugha ya kiswahili mzizi umegawanyika katika aina kuu mbili ambazo ni
i) Mzizi huru
Mfano. Mama na Baba pia Mjomba
ii) Mzizi tegemezi
Mfano Cheza → Chez-
Lima → Lim-
Piga → Pig

Kielelezo 3.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua kwa usahihi *ngeli za majina, mofimu, kirai, sentensi na mzizi*.

Watahiniwa wengine asilimia 33.4 walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kufafanua baadhi ya dhana za kisarufi bila utoshelevu hususani kwa kutotumia mifano katika ufafanuzi wao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana katika vipengele (a), (b), (c) na (d) kwa usahihi lakini hakutumia mifano ili kufafanua maana hizo. Pia katika kipengele (e), mtahiniwa alishindwa kabisa kutoa maana ya *mzizi* kwa kueleza kuwa; *ni neno ambalo linaweza kubeba mofimu zaidi ya moja ili kuleta maana kamili ya neno* badala ya kuelezea kuwa ni *sehemu ya neno isiyobadilika baada kuondolewa viambishi*. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 3.2


3. a. Ngali za magina ni namna ya kuwa ka magina kaika makundi yana-yoyoana au kuuwiana.
mfano: Kisu → Visu ni ngali ya Ki-Vi
Miti umayungika → M-T.
Miti imayungika

b. Mofimu ni kipashio kidogo cha kitsi mu chanye maana kisarufi/kilaksia
mfano:- Mofimu ma-ma inaunda nano mama
→ Ku, ki, ji hizi ni mofimu

c. Kirai ni aina ya kungo yanye nano mo ja au zaidi lakini haina muundo wa kiima na kiarifu.

d. Sankansi ni mpangilio au kifungu cha manano kinachoka kaariga kamili na kinaunduwa na muundo wa kiima na kiarifu.
Mfano:- Baba / anaendesha gari
K / A
→ Msichana / amepanda
K / A



3. a. Mzizi ni neno ambalo linaweza
kubeba mofimu zaidi ya moja ili kule
ta maana kamili ya neno.
Mfano: Mzizi chaz unaweza kuwa
Anachaza, Watachaza.

Kielelezo 3.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kutoa ufafanuzi wa *ngeli za majina, mofimu, kirai, sentensi na mzizi* bila utoshelevu.

Watahiniwa wachache, asilimia 10.3, waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kushindwa kufafanua dhana za kisarufi walizopewa. Kati yao, asilimia 0.2 walishindwa kufafanua dhana zote na kupata alama 0. Kielelezo 3.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa ufafanuzi wa dhana za kisarufi katika vipengele vyote vitano.

Kielelezo 3.3



3 a) Ngeli ya majina.
→ Ni maneno yanayounda na kuta-
mbulisha jina ya vitu mbalimbali

b. Mofimu
→ Ni herufi / neno ambalo linaunganishwa
na silabi ili kuleta muundo halisi na maana
ya neno ambayo inaweza ikawa tegemezi au thuru
Mfano

c). Kirai
→ Ni herufi ya katika ambayo inawakili
sha kitu.

d) Sentensi – ni muunganiko wa maneno.

e) Mzizi – ni herufi terye chanzo cha neno
au Sentensi

Kielelezo 3.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua *ngeli za majina, mofimu, kirai, sentensi na mzizi* na kupata alama hafifu.

2.3.2 Swali la 4: Matumizi ya Sarufi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* na lililenga kupima maarifa. Swali lilimtaka mtahiniwa atumie mifano kutoka katika lugha ya Kiswahili kutoa hoja tano zinazobainisha tofauti kati ya *mofimu tegemezi* na *silabi*. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 10.

Watahiniwa wachache (4,581) sawa na asilimia 22.4 walijibu swali hili kwa kuwa lilikuwa la kuchagua. Kiwango cha kufaulu kilikuwa cha wastani, kwani asilimia 47.1 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.

Jedwali Na 2: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Watahiniwa	Asilimia ya Watahiniwa
0.0 - 3.0	2,422	52.9
3.5 - 5.5	1,607	35.1
6.0 - 10.0	552	12.0

Zaidi ya nusu ya watahiniwa (52.9%) waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kushindwa kubainisha tofauti kati ya *mofimu tegemezi* na *silabi*. Watahiniwa hao walikosa maarifa mahsusi kuhusu mofimu na silabi za Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha tofauti za mofimu tegemezi na silabi kwa kigezo cha *dhima* na *idadi ya herufi zinazounda silabi/mofimu hizo* kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini 0 hadi 3 katika swali hili.

Kielelezo 4.1



4. Ni vehemu muhimu ya neno na haiwezi kubadilishwa katika Sentensi mfano neno baba haliwezi kubadilishwa na kuwa gabb au abab kwani halita leta maana.
Hivyo Silabi na mofimu zinatofautiana lakini zote hudumika katika lugha na hufanana kiasi fulani kama zote zinaundwa na fonimu.

Kielelezo 4.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutofautisha mofimu tegemezi na silabi kwa kuzingatia *maana aina za vipashio* na *uwezo wa kuambishwa* badala yake akatofautisha dhana hizo kwa kwa kigezo cha *dhima* na *idadi ya herufi zinazounda silabi/mofimu* na kupata alama hafifu.

Watahiniwa wengine, (35.1%) waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kubainisha tofauti pungufu kati ya mofimu tegemezi na silabi kama ilivyotakiwa. Watahiniwa hao waliweza kubainisha baadhi ya tofauti kwa usahihi kama vile; *tofauti inayotokana na maana* au *kipashio cha kifonolojia ama kimofolojia* lakini wakashindwa kuelezea tofauti nyingine kama vile *aina za vipashio* na *uwezo wa kuambishwa*. Kielelezo 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa majibu yasiyojitosheleza katika kutofautisha mofimu tegemezi na silabi.

Kielelezo 4.2

4. Zifuatazo ni tofauti kati ya mofimu tegemezi na silabi.
Katika maana, mofimu tegemezi ni aina ya mofimu ambayo haiweri kusimama peke yake katika neno ikaleta maana LAKINI, Silabi ni fungu la sauti ambalo linaweza kutamkwa mara moja na kwa pamoja.
Katika neno kila mofimu tegemezi inakazi yake. Mfano katika neno a-na-cher-a a-huonesha nafsi, na-huonesha wakati uliopo, a-huonesha kiambishi tamati LAKINI katika silabi si kila silabi inakazi yake katika neno. Mfano ba.
Mofimu tegemezi zinaweza kuvunjwa vunjwa katika neno. Mfano katika neno a-na-lim-a LAKINI silabi haziweri kuvunjwa vunjwa katika neno Mfano huweri ukavunja neno ba-ba (baba).
Si kila neno linakuwa na mofimu tegemezi kwani kunamaneno ambayo ni huru hayahitaji mofimu tegemezi mfano wa maneno hayo ni baba, mama, shangazi, juma,-



4. Mjomba LAKINI kila neno ni
larima liwe na silabi na
silabi hizo ni zaidi ya moja.
Mofimu tegemezi haziwezi
kusimama peke yake zikaleta
maana kwani zinahitaji
mofimu tegemezi ili kukami-
lisha maana zake za msingi.
Mfano mofimu a-haiwezi
ikasimama peke yake na
kuleta maana inahitaji msaada
kutoka mofimu tegemezi LAKINI
Muunganiko wa silabi
unaweza kusimama peke yake
na kukamilisha maana.
Mfano silabi batba zikiunga-
nishwa zimeleta maana zinau-
nda neno baba ambalo katika
kiswahili sanifu lina maana
ya mzazi wa kiume.
Hivyo basi hizo zilizotajwa
ndio tofauti za msingi ambazo
zinaweza kutofautisha mofimu
tegemezi na silabi.

Kielelezo 4.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja zisizojitosheleza katika kutofautisha mofimu tegemezi na silabi.

Aidha, asilimia 12.0 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Miongoni mwao, asilimia 1.4 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10 kwa kuwa walitoa hoja zilizojitosheleza katika kutofautisha mofimu tegemezi na silabi kwa kutumia *maana, aina za vipashio* na *uwezo wa kuambishwa* kwa dhana hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha tofauti nne kwa usahihi kati ya mofimu tegemezi na silabi na kutoa mifano inayoshadidia tofauti hizo, japokuwa alishindwa kutoa mfano katika hoja moja na hivyo kutopata alama zote. Kielelezo 4.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwa kubainisha kwa usahihi tofauti kati ya mofimu tegemezi na silabi.

Kielelezo 4.3

4. Tofauti kati ya mofimu tegemezi na silabi, kwa mifano:

i) Mofimu tegemezi ni mofimu ambazo haziwezi kusimama pekee katika neno na kutoa maana iliyo kusudiwa mfano; Ana-, -a, si- na kadhalika.

Wakati;

Silabi ni tamko katika neno linalotamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti mfano; Ba-ba, ka-ka, Da-da.

4. ii) Mofimu tegemezi inaweza kupachikwa katika mzizi wa neno ili kutoa neno lenye maana mfano; A-na-chez-a ambapo chez ni mzizi.

Wakati,

Silabi ni sauti za namna moja na hutokea sehemu yoyote ya neno bila kujali ni mzizi au siyo mzizi wa neno, kwa mfano; neno anacheza silabi ni a-na-che-za.

iii) Silabi inauwezo wa kuugawa mzizi wa neno katika vipande vidogo ambayo vinaweza kutamkwa kwa mfano; mzizi -imb- kwenye a-na-imba -chez- kwenye a-na-che-za.

Wakati

Mofimu tegemezi haziwezi kugawa mzizi wa neno kwani havisimami pekee kuleta maana bali vinategemea viambishi vingine kupachichwa ili zileta maana pale neno linapojengwa na mofimu tegemezi

iv) Silabi zipo za aina mbili ambazo ni silabi huru ambazo hufunguliwa au huishia na irabu na silabi funge ambazo huishia na konsonati mfano; Ba-ba-Irabu (silabi huru)

Wakati.

Mofimu tegemezi ni aina ya mofimu ambapo mofimu ni neno au kipande cha neno chenye maana kisanefi na kileksika ambapo mofimu tegemezi imejidhihirisha katika utegemezi kwani haziwezi kusimama pekee na kutoa maana iliyokusudiwa.

v) Katika uambishaji kila kiambishi cha mofimu tegemezi huwa na kazi fulani kwa mfano neno anapika ambapo hutengwa au huambishwa A-na-Pik-a hapa mofimu



4 tegemezi ni A-kiambishi awali nafsi ya tabi umoja, -na- kuonyesha wakati au njeo iliyopo, -a ni kiambishi tamati maana kwa sababu kinajenga mzizi waneno pika hivyo hii ni sifa ya mofimu tegemezi Wakati,
Silabi katika utengaji wake huonyesha namna au tofauti katika utamkaji unaofanyika katika maneno mbalimbali lakini vile kuonyesha kazi ya kila kiambishi kama iliyo kwa mofimu tegemezi kwa mfano neno anapika litatenguwa kama A-na-pi-ka hivyo kuonyesha tofauti katika matamshi ya neno hilo.

Kielelezo 4.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetofautisha mofimu tegemezi na silabi kwa usahihi na kupata alama za juu.

2.3.3 Swali la 5:Utumizi wa Lugha

Swali lilitoka katika mada ya *Utumizi wa Lugha* na lilipima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja tano zinazoelezea umuhimu wa kuzingatia uhusiano baina ya wahusika wakati wa kutumia lugha na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Watahiniwa 6,684 sawa na asilimia 32.7 ya watahiniwa wote walifanya swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilijibiwa vibaya ambapo asilimia 13.9 pekee ya watahiniwa ndio waliofaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika swali hili kiasilimia.



Chati Na. 3: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 86.1 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kukosa maarifa kuhusu umuhimu wa uhusiano wa wahusika katika kutumia lugha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile; *mada ya mazungumzo, mazingira, umri, ujira/ajira na kutumia lugha kwa ufasaha* (mambo ya kuzingatia katika lugha) badala ya kuelezea umuhimu wa kuzingatia uhusiano baina ya wahusika katika kutumia lugha kama vile *kuonyesha uhusiano mwema, kuzuia mmonyoko wa maadili, kuepusha migogoro na kuleta heshima miongoni mwa watu*. Kielelezo 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali na kupata alama hafifu.

Kielelezo 5.1



5 Kwa nini ni Muhimu Kuzingatia uhusiano baina ya
wahusika wakati wa kutumia lugha? hoja tano
Wahusika ni watu ambao huzanya jambo zulani
kwa kukutana na kujadili suala zulani ambao
katika wahusika unaweza ukawa uhusika wa
Baba na Mtoto ake, Mwalimu na Mwanazunzi
au Mtu na Mpenzi wake hivyo ni Mhimu
kuzingatia uhusiano baina ya wahusika wakati wa
kutumia lugha kwa kuzuatana na hoja zizuatazo
Mada ya Mazungumzo, katika Mada ya
Mazungumzo ina tegemea na uhusiano baina ya
wahusika ambapo mada hiyo yaweza kuwa
kati ya Mwalimu na Mwanazunzi katika kuj
adili masomo shuleni na pia mada iyo
yaweza kuwa Mtu na mpenzi wake kuhusia
na na Mapenzi yao hivyo uhusiano baina
ni Mhimu.
Mazingira hutozautiana, pia ni Mhimu kuzing
atia uhusiano baina ya wahusika katika kutumia
lugha kwa sababu ya Mazingira kutozautia na kwa
Mzano katika Mazingira ya hospitalini uhusiano
huo ni wa Mgonjwa na daktari na shuleni ~~na~~
ni Mwalimu na Mwanazunzi hivyo ni Mhimu
kuzingatia uhusiano baina ya wahusika katika
Matumizi ya lugha.
Umri, katika kuangalia uhusiano wa wahu
sika ni dhahiri kigezo cha umri bayana ya wahusi
ka hutozautiana na hivyo kumzanya mzungumzaji
atambuze huyu mhusika ni mkubwa kwangu au –
mdogo kwangu,



Kielelezo 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza mambo muhimu ya kuzingatia katika kutumia lugha badala ya kueleza umuhimu wa uhusiano wa wahusika katika kutumia lugha na hivyo kupata alama hafifu.

Aidha, watahiniwa wachache, asilimia 11.1 walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kwa kuwa walitoa majibu yasiyojitosheleza. Baadhi ya watahiniwa walitoa majibu sahihi kwa baadhi ya hoja na kushindwa katika hoja nyingine kuhusu umuhimu wa uhusiano baina ya wahusika katika kutumia lugha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile; *husaidia kuonyesha uhusiano mwema, kuzuia mmonyoko wa maadili na kumfanya mtu awe na heshima* na kutoa hoja isiyo sahihi kama, *kuendeleza ujuzi wa lugha* na kupata alama za wastani. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyojitosheleza.

Kielelezo 5.2

5. Utumizi wa lugha; Ni namna ya kutumia lugha kulingana na mila na desturi za jamii ha uhusiano baina ya wahusika ni namna ya kutumia lugha kulingana na nani unaongea naye.

Kuna umuhimu wa kuzingatia uhusiano baina ya wahusika wakati wa kutumia lugha kutokana na hali zifuatazo.

Husaidia kukuza uhusiano mwema baina ya watu; Wakati wa kutumia lugha kama mtu anatumia lugha kwa kuzingatia uhusiano baina ya wahusika inaweza kwaidia watu kukuza uhusiano mwema kwa sababu lugha inayotumika Mlongoni mwa watu wa rika moja ni tofauti na lugha ya baba na mtoto.

Inamfanya mtu kuwa na tabia nzuri; Pia wakati wa utumizi wa lugha kama kutakuwa na uhusiano baina ya wahusika inaweza kwaidia katika kumfanya mtu kuwa na tabia nzuri kwa sababu mtu huyo ndiye wa kwama kutumia lugha kwa kuangalia ni nani anaongea naye kwa mfano baba, mama au mtu wa rika lako.

Huweza kuendeleza ujuzi wa lugha; kutokana na watu kutumia lugha kulingana na jinsi inavyotakiwa kutumika kwa kuangalia uhusiano baina ya wahusika huweza kuendeleza lugha Mlongoni mwa watu wakati wa kutumia katika mawasiliano ya kila siku.

Inamfanya mtu kuwa na heshima; kwani wakati wa mazungumzo mtu huwa anatumia lugha ambayo inafaa katika mawasiliano baina yao. Hivyo kutokana na kuzingatia uhusiano baina ya wahusika inawafanya watu kuwaheshimu wakubwa kwa wadogo.

Inazuia mmomonyoko wa maadili; kwa mfano matumizi ya lugha viyofaa kwa mhusika ndio maana ni muhimu kuzingatia uhusiano baina ya wahusika ili watu wawezo kuwa na maadili inayotakiwa.

Hivyo basi; kuna umuhimu mkubwa wa kuzingatia uhusiano baina ya wahusika ili watu wawezo kutumia lugha kama inavyotakiwa.

Kielelezo 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyojitosheleza katika kuelezea umuhimu wa uhusiano baina ya wahusika katika kutumia lugha na kupata alama za wastani .

Watahiniwa wachache, asilimia 2.8 walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Miongoni mwao, asilimia 0.2 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10 kutokana na kutoa hoja zilizojitosheleza kuhusu umuhimu wa kuzingatia uhusiano baina ya wahusika wakati wa kutumia lugha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile; *kuepusha migogoro mbalimbali, kuheshimiana baina ya mtu na mtu, kutofautisha rika moja na jingine na kuimarisha maadili mazuri katika jamii*; lakini katika hoja yake ya kwanza alieleza; *ili kuleta tofauti kati ya mtu na mtu*; hoja ambayo si sahihi. Kielelezo 5.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili japokuwa hoja yake ya kwanza haikuwa sahihi.

Kielelezo 5.3

05 Katika kutumia lugha ni muhimu kuzingatia uhusi
ano baina ya wahusika kwa sababu zifuatazo:-
(i) Ili kuleta utofauti baina ya mtu na mtu; katik
a kuzingatia uhusiano wa wahusika katika kutumi
a lugha inaweza au inatofautisha mtu na mtu
Mfano; Mwanafunzi na Mwalimu hapa mja kw
a mja Mwanafunzi atacnyesha utofauti katika mazun
gumzo yao na Mwalimu.
(ii) Huweza kuepusha migogoro mbalimbali katika
Jamii; pia kuzingatia uhusiano wa wahusika katik
a kutumia lugha huepusha migogoro Mfano Huwezi
ukaongea na mwalimu kama mwanafunzi mwenzio;
(iii) Huwezesha kuheshimiana baina ya mtu na
mtu; pia katika kuzingatia uhusiano ~~baina~~ baina



05. ya wahusika kuleta heshima kwa sababu kuweza kuka
ta mazoea na lugha za maajabu. Mfano Mtoto na Baba
ake, Mwanafunzi kwa Mwalimu, na pia vijana kwa vijana
(iv) Huweza kutofautisha kati ya rika moja na
jingine; pia katika kutumia au kuzingatia uhusia
no baina ya wahusika huweza kutofautisha baina ya
rika moja na jingine. Mfano. Kijana kwa wazee.
Mtoto kwa Baba hata ~~mw~~ Mwanafunzi kwa Mwalimu.
(v) Huimarisha maadili mazuri katika jamii.
pia katika kuzingatia uhusiano wa wahusika katika
kutumia lugha huweza kuimarisha maadili katika
jamii. Mfano; Kijana anapoongeza na Mzee au Baba
yake kutumia lugha yenye maadili mazuri pia hata
Mwanafunzi anapoongea na Mwalimu kutumia lugha
yenye maadili mazuri.
Hivyo basi uzingatiaji wa uhusiano baina ya
wahusika ni muhimu katika jamii.

Kielelezo 5.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kuelezea umuhimu wa kuzingatia uhusiano baina ya wahusika wakati wa kutumia lugha kama vile; *kuepusha migogoro, kuleta heshima baina ya mtu na mtu, kutofautisha rika moja na jingine na kuimarisha maadili mazuri katika jamii* .

2.3.4 Swali la 6: Utumizi wa Lugha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utumizi wa Lugha* na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa maana tano za neno "pasi" na kutunga sentensi moja kwa kila maana. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilikuwa la kuchagua na lilifanywa na watahiniwa 10,109 sawa na (49.5%). Swali lilijibiwa vizuri ambapo asilimia 91.8 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kiasilimia**.**



Chati Na. 4: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 57.4 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10 kutokana na kutoa kwa usahihi maana za neno "pasi" kama vile; *kifaa cha kunyooshea nguo, tendo la kurushiana mpira, kufaulu mtihani, bila ya kuwa na sababu na hati ya kusafiria*. Aidha, watahiniwa hao walitunga kwa usahihi sentensi zinazohusiana na maana hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa kwa usahihi maana nne za neno “pasi” na kuzitungia sentensi japokuwa hoja yake ya mwisho haikuwa sahihi kwa kuwa alitoa maana ya neno “pasi” kama *ruhusa ya kusafiria* badala ya *hati ya kusafiria*. Kielelezo 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa maana sahihi nne za neno "pasi" na kuzitungia sentensi kama ilivyotakiwa.

Kielelezo 6.1


6 Maana za neno pasi
-> pasi ni chombo cha kunyooshea nguo
• Baba yangu amenunua pasi ya umeme
-> pasi ni kitendo cha kunyosha nguo
• Mama ameniomba nipige pasi nguo zake
-> pasi kitendo cha kufaulu vizuri kahita masomo
• Mwajuma anategemea kupata pasi muri kahita masomo yake.
-> Pasi kitendo cha kupiga mpira kwenda kwa mtu mwingine
• Juma amepiga pasi ndefu kwelekea golini' na kisha kusababisha goli
-> Pasi kinachoonesha ruhusa ya kusafiria
• Mwajuma amepewa pasi ya kusafiria na mlanyemi wa elimu.

Kielelezo 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa maana nne sahihi za neno “pasi”japokuwa katika maana ya mwisho aliandika *ruhusa ya kusafiria* badala ya hati ya kusafiria.

Watahiniwa wengine (34.4%) walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kutoa majibu yaliyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika majibu yake, alitoa maana tatu sahihi za neno *pasi* katika (i, ii na iv) lakini akatoa

maana mbili zisizo sahihi katika (iii na v) na hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyojitosheleza.

Kielelezo 6.2


6. i. Pasi - ni kigoa lchombo cha kunyooshaa Nguo.
Mgano ÷ Mungu wangu!! Pasi imaungua nguo sigui nitaandaa kasho shule.

ii. Pasi - ni kitando cha kugaulu mikih ani.
mgano ÷ Nimapasi na alama nzuri za kuandalaa chuo kikuu.

iii. Pasi - ni kitando cha kumpa mtu kitu kilicho mbali.
mgano ÷ Dada naomba unipasia hiyo sahani hapo mezani

iv. Pasi - ni kitando kinachotumiwa na wachezaji wa mpira.
Mgano ÷ Juma, Juma nipasia hapa, hapa.

v. Pasi - ni kama njia
mgano ÷ Jamani naombani nipasi hapo maana mmasimama njiani.

Kielelezo 6.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa maana tatu za neno "pasi" kwa usahihi na kutoa maana zisizo sahihi kama *kitendo kinachotumiwa na wachezaji* na *kama njia* na kupata alama za wastani.

Asilimia 8.2 ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kushindwa kutoa maana na kutunga sentensi tano za neno *pasi* kutokana na kukosa maarifa ya maneno yenye maana zaidi ya moja (visawe). Baadhi ya watahiniwa walitoa maana za neno "pasi" kama; *neno linalotoa maana kamili, lisilotoa maana kamili, neno linaloonesha amri, hali ya kuonesha utendaji, hali ya kuonesha ukanushi au uyakinishi* na wengine walitoa maana zisizo na uhusiano wowote na neno hilo na kupata alama 0. Kielelezo 6.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa maana za neno “pasi” kama kifaa au kitendo bila kuhusianisha na maana ya msingi ya kitendo au kifaa hicho.

Kielelezo 6.3


6. Maana ya neno pasi.

i/ Pasi kama kifaa.
- Ninenunua pasi yangu.

ii/ Pasi. kuacha kula chakula kwa muda.
Mfano.
Leo nitapiga pasi ndefu.

iii/ Pasi kama kitendo.
Mfano.
Naomba ni pasi nguo zangu.

iv/ Pasi kuonyesha wakati uliopita.
Mfano.
Jana nili piga pigo pasi ndefu kwanza a asubuhi hadi jioni.

v/ Pasi kama kitendo cha kupitisha.
Mfano.
Ni pasie hilo chungwa hapa.

Kielelezo 6.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa maana hata moja ya neno "pasi" na kupata alama 0.

2.4 SEHEMU C: UTUNGAJI

2.4.1 Swali la 7: Utungaji

Swali lilitoka katika mada ya *Utungaji* na mada ndogo ya *Uandishi wa Matangazo* na lililenga kupima uundaji. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika tangazo kuhusu katizo la safari ya ndege kutoka Songea kwenda Zanzibar na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilikuwa la lazima ambapo asilimia 99.9 ya watahiniwa walilijibu. Miongoni mwao, asilimia 98.7 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha ya kuandika tangazo kwa kuzingatia vigezo muhimu. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia**.**



Chati Na. 5: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 88.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Kati yao, asilimia 18.3 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 20 kwa kuwa waliweza kuandika tangazo kwa kuzingatia; *kichwa cha tangazo; aina na namba ya ndege; siku na tarehe ya safari iliyoahirishwa; mahali ndege ilikokuwa inaelekea; sababu ya kuahirishwa kwa safari; tarehe, siku na muda wa safari mpya, kuomba radhi kwa usumbufu; saini, jina na cheo cha mwandishi*. Kielelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika tangazo kwa usahihi.

Kielelezo 7.1



7- TANGAZO!.

KATIZO LA USAFIRI WA NDEGE

NAMBA TY JET 343

SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA LINAWAFANGA ZIA ABIRIA KUWA KUJAKUWA NA KATIZO LA USAFIRI WA NDEGE NAMBA TY JET 343 ILIYO KUWA IFANYE SAFARI YAKE TOKA SONGEA KWENDA ZANZIBAR SIKU YA IJUMAA TAREHE 25/5/2018 SAA 12 ASUBUHI. ~~KUWA~~ SAFARI HIYO ITAFANYIKA JUMAPILI TAREHE 27/05/2018 SAA 8 MCHANA. MABADILIKO HAYA YANATOKANA NA KUCHAFUKA KWA HALI YA HEWA ANGANI.

SHIRIKA LINAWAPA POLE ABIRIA WOTE KWA USUMBUFU UTAKAO JITOKEZA.

IMETOLEWA NA AFISA HABARI WA SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA.

~~KATIZIKI~~

KUDURA RIZIKI.

Kielelezo 7.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika tangazo la kuahirishwa kwa safari ya ndege na kupata alama za juu.

Watahiniwa wachache (9.8%) walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutozingatia baadhi ya vipengele vinavyohitajika katika uandishi wa tangazo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika tangazo lisilojitosheleza kutokana na kuacha baadhi ya vipengele muhimu katika uandishi wa tangazo kama vile; *kichwa cha tangazo, saini ya mtoa tangazo na kutoomba radhi kwa abiria kutokana na katizo la safari*. Aidha, mtahiniwa huyo aliandika jina la mtoa tangazo mwanzoni badala ya mwishoni mwa tangazo kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu muundo wa tangazo. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika tangazo lisilojitosheleza na kupata na alama za wastani.

Kielelezo 7.2



07. TANGAZO! TANGAZO! TANGAZO!

KWA MAJINA NAITWA KUDURA RIZIKI, NI AFISA HABARI WA SHIRIKA LA NDEGE NCHINI TANZANIA! NAPENDA KUWATANGAZIA ABIRIA WOTE WANAOSAFIRI NA NDEGE NAMBA TY JET 343 INAYOTAKA SONGEA KWENDA ZANZIBAR SIKU YA IJUMAA TAREHE 25/5/2018 SAA 12 ASUBUHI, KUWA SAFARI HIYO ITAFANYIKA SIKU YA JUMAPILI TAREHE 27/05/2018 SAA 8 MCHANA KUTOKANA NA MABADILIKO NA AA YALIYOTOLEWA NI KWASABABU YA KUCHAFUKA KWA HALI YA HEWA ANGANI EWE ABIRIA WETU TAFADHALI KWA USUMBUFU ULIOJITOKEZA.

Kielelezo 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika tangazo la kuahirishwa kwa safari ya ndege bila kuzingatia muundo na baadhi ya mambo muhimu katika uandishi wa tangazo na kupata alama za wastani.

Watahiniwa wengine (1.3%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama za chini kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na uelewa mdogo wa uandishi wa tangazo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika barua ya kikazi kwa kuwa alishindwa kutofautisha tangazo na barua za kikazi. Kielelezo 7.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuandika tangazo na kupata alama 0.

Kielelezo 7.3



7.

Shirika la Ndege Tanzania,
B.ox, 320,
Zanzibar,
25/5/2018.

Usafiri wa ndege,
B.ox. 274,
Sogea,
27/05/2018.

MAHUSU: TANGAZO LA ABRIA LA KUSAFIRI KWA NDEGE:

Husika na mada hiyo hapo juu. ~~mimi~~ Ninafurahia ya kutuarifu kuwa kumetokea tatizo la Ndege kudefika huko iliyoondoka siku ya jumaa tarehe 25 25/5/2018 saa 12 asubuhi

Kielelezo 7.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika tangazo la kuahirishwa kwa safari ya ndege kwa muundo wa barua ya kikazi na kupata alama 0.

2.5 SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI

2.5.1 Swali la 8: Ukuaji wa Lugha ya Kiswahili.

Swali lilihusu mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* na mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania* na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa kujadili changamoto sita zinazoikabili lugha ya Kiswahili nchini Tanzania na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Watahiniwa wengi (78.7%) walijibu swali hili lililokuwa la kuchagua, ambapo miongoni mwao, asilimia 91.2 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani kuanzia alama 7 hadi 19.5. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kiasilimia.



Chati Na. 6: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Zaidi ya nusu ya watahiniwa, asilimia 53.1 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kujadili baadhi ya changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili nchini kwa usahihi na kushindwa kujadili changamoto nyingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijadili kwa usahihi changamoto kama vile; *uhaba wa fedha, Kasumba kwa wasomi na wanasiasa kuidharau lugha ya Kiswahili na sera ya lugha ya nchi kulegalega*, lakini akajadili changamoto nyingine ambazo hazikukidhi matakwa ya swali kama vile; *ukosefu wa vitabu vya kujifunzia, uhaba wa wataalamu na kuwepo kwa lugha rasmi* na hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kujadili baadhi tu ya changamoto na kuacha nyingine.

Kielelezo 8.1

08. Lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zenye kutoa maana zilizoteuliwa na jamii ya watu fulani ili zitumike katika mawasiliano. Lugha ya kiswahili nchini Tanzania ndiyo lugha kuu ya mawasiliano na ya taifa. Licha ya kuwa lugha ya taifa lukubwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo;

Uhaba wa fedha za kuchapisha majarida kwa ajili ya makongamano ya kiswahili nchini Tanzania bado tatizo la fedha hulikumba suala la kiswahili kwa sababu ya ukosefu wake watu hushindwa kuchapisha na kuandaa makongamano ya kiswahili ili kukikuza zaidi.

Ukosefu wa vitabu vya kujifunzia lugha ya kiswahili nchini Tanzania bado vitabu vya kiswahili ni changamoto sana kwenye shule zetu hivyo kukwami sha zoezi la ufundishaji ili watu na wana funzi wote kuweza kuitambua vyema.

Uhaba wa wataalamu wa lugha ya kiswahili ili ni tatizo kubwa watu wote au wengi nchini Tanzania huzungumza kiswahili lakini wataalamu au mahiri wenye ujuzi na utadi zote za lugha ni wachache hivyo watu huzidi kuidumaza lugha kwa kuongea kiswahili kisicho fasaha kabisa.

Kasumba wasomi na wanaviana huidharau sana lugha ya kiswahili hivyo huzidi kudumaa kwa sababu wao ndiyo

08. wanaotakiwa kuzidi kuieneza kote lakin
i baada ya kusoma na kujifunza lugha-
mbalimbali kama kiingereza, kifaransa-
na kiarabu huona kiswahili hakuna maa
na tena.

Sera ya nchi kulegalega nchini
Tanzania sera ya kiswahili katika elimu
nishule za msingi kiswahili kitumike
kama njia ya mawasiliano na kufundishia
na somo la kiingereza ndiyo halifundishwi
kwa kiswahili na kuanzia elimu ya-
sekondari kiswahili hufundishwa kama-
somo moja tu lakini tunaona kuwa sera-
hulegalega kwa sababu kuna wakati Tanz
ania ilitaka kubadili mfumo na shule-
zote za msingi kutumia kiingereza na
baadae wakaacha pia ilikuja sera ya kuwa
kiswahili kitumike hadi shule za sekond
ari na elimu ya juu lakini ilishindikana
hivyo bavi serikali inachangia ugumu wa
kuendelea kiswahili.

Kuwepo kwa lugha rasmi mbali
mbali nchini kama hapa Tanzania kuna-
lugha ya kiswahili na kiingereza na zote
ni lugha rasmi ambazo hutumika katika
shughuli za kiofisi, bungeni na rasmi.-
Hapa kiingereza huleta changamoto kwa
kiswahili kwa sababu huziti kukua na
kupata wasomaji na watumiaji wengi-
kuliko kiswahili.

Kielelezo 8.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa jibu lisilojitosheleza kwa kutoa baadhi ya changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili kwa usahihi na kupata alama za wastani.

Asilimia 38.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri na kupata alama kuanzia 12 hadi 19.5. Miongoni mwao, asilimia 1.9 walijibu vizuri na kupata alama za juu kuanzia 17 hadi 19.5 kwa kuwa waliweza kujadili kwa usahihi changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili nchini Tanzania kama vile; *kasumba ya kudharau lugha, mfumo wa elimu, upinzani kutoka lugha za kigeni, sera ya lugha kulegalega, kukosekana kwa fedha za*

kuendeleza shughuli za ukuzaji na *watanzania wengi kutokuwa na utamaduni wa kujisomea vitabu*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijadili kwa usahihi changamoto nyingi zinazoikabili lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Hata hivyo, mtahiniwa huyo alitoa hoja ya *uhaba wa wataalamu* ambayo si sahihi, kulingana na hali ya sasa ya lugha ya Kiswahili. Kielelezo 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejadili kwa usahihi changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili nchini Tanzania kulingana na matakwa ya swali.

Kielelezo 8.2

8 Kiswahili ni lugha ambayo inatumika nchini Tanzania ikiwa lugha ya Taifa. Lugha hii ya Kiswahili ilisanifishwa kutoka katika lahaja ya Kiunguja baada ya Kiunguja kuteuliwa mnamo mwaka 1928 kama lahaja ya usanifishaji katika mkutano uliohusisha magavana na wanaisimu kutoka Tanganyika, Kenya na Uganda mjini Mombasa. Tangu kusanifishwa kwa lugha ya Kiswahili na kuteuliwa kawa lugha ya Taifa nchini Tanzania kuna changamoto mbalimbali zinazo ikabili lugha hii kama ifuatavyo.

Uhaba wa wataalamu; Lugha ya kiswahili inakabiliwa na uhaba wa wataalamu nchini Tanzania ambao wangesaidia katika kufanya tafiti mbalimbali juu ya lugha ya Kiswahili pia katika kuiboresha sarufi ya lugha hii ya Kiswahili.

Kasumba ya kuidharau lugha; Miongoni mwa watanzania kuna baadhi wanaoidharau lugha ya kiswahili na kuona kama lugha ya tabaka la chini hivyo kupelekea ukuaji wake kulegarega. Baadhi ya wanaoidharau lugha hii ni pamoja na wasomi wengi wusuani ambao wameipata elimu ya juu sana.

Mfumo wa elimu; Nchini Tanzania lugha ya Kiswahili inakumbana na changamoto kutokana na mfumo wa elimu namna uliyo ambapo lugha ya Kiswahili inatumika sana katika elimu ya msingi lakini katika elimu ya juu kuanzia sekondali lugha ya - Kiswahili inatumika tu kama lugha au -



8 somo mojawapo kama yaliyo masomo mengine na sio lugha ya mawasiliano katika elimu ya sekondari.

Upinzani kutoka katika lugha za kigeni; huu ni mirongoni mwa matatizo yanayoikumba lugha ya Kiswahili nchini Tanzania mfano baadhi wanaona lugha ya Kiswahili kuwa itumike katika ngazi ya chini mfano katika elimu na kushauri kingereza na kitumike katika mambo makubwa mfano katika kufundishia elimu ya juu.

Sela ya lugha kulegalega; lugha ya Kiswahili nchini Tanzania inakumbana na changamoto ya sela kulegalega au kutokuwa imara mfano baazi ya sela ambazo huanzishwa kwa lengo la kuikuza lugha ya Kiswahili huishindwa kutokana mkazo katika utekelezaji wake na mwishowe kupelekea Kiswahili kudumaa.

Kukosekana kwa fedha za kutosha katika kuendeleza shughuli za ukuzaji na uenezaji wa lugha ya Kiswahili; Pia lugha ya Kiswahili inakumbana ~~ka~~ tatizo la kifedha mfano katika kurabibu shughuli zinazofanywa na vyombo mbalimbali vya ukuzaji na uenezaji wa lugha nchi kama vile TUKI, BAKITA na UKUTA.

Kutokana na changamoto huzo zinazoikumba lugha ya Kiswahili selikali inabidi itilie mkazo katika utumiaji wa lugha ya Kiswahili kama nyenzo ya mawasiliano katika ngazi zote, pia kuwahimiza watu kuacha kusumbu ya kuizaau lugha ya Kiswahili pia kuandaa sela madhubuti kuhusu lugha na kufanyiwa utekelezaji kama inavyostahili.

Kielelezo 8.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejadili kwa usahihi changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili nchini Tanzania na kupata alama za juu.

Aidha, asilimia 8.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa maarifa kuhusu changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile; *makosa ya kisarufi, utata katika sentensi au neno, kuongea bila ya kuzingatia muktadha,*

kutumia misimu, vinasa sauti na uchanganyaji wa maneno ya lugha mbili kwa wakati mmoja; majibu ambayo hayana uhusiano wowote kuhusu changamoto zinaziokabili lugha ya Kiswahili. Pia, alitoa hitimisho lisilokidhi kabisa matakwa ya swali na hivyo kupata alama 0. Kielelezo 8.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujadili changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.

Kielelezo 8.3


8 Kiswahili nilugha yataifa ya nchi ya Tanzania kuanzia ilipochaguliwa lahaja ya kiunguja. Kuna changamoto mpinzi sana katika lugha ya Kiswahili hapa nchini Tanzania na nikama zifuatazo

Makosa ya kisarufi, hii nichangamoto mayokabili Tanzania katika nchiyake kwa kupitia makosa ya kimantiki ya sarufi mfano wa neno mazingira mtu anatamka mazingila ~~baadaya~~ ~~a~~ hukosea tu.

8 Utata katika sentensi au neno, hili
nalo nitatizo au changamoto zinazo ikabili lugha
ya kiswahili hapa nchini Tanzani ~~mazo~~ mfano
mzuri wa Utata katika neno ni pale mtu anapo
po ~~wa~~ mwambia mtu nipe kibao neno kibao
lina maana zaidi ya moja kwahiyo hili ni
changamoto

~~Kuto~~ Kuongea bila yakuto zingatia mukut
adha, kuna baadhi ya watu wanaongea bila ya
kutozingatia mazingira aliyokuwepo na ana
kuwa anatumia mitindo ya lugha (Rejesta)
kwa hiyo na hii nichanga moto mojawapo.

Kutumia Misimu, yani kuna watu
wanatumia maneno yasiyo rasmi yani sio
sanifu katika lugha yanayo zushwa na kufa asa
mtu anakuwa analeta katika lugha. ~~pasaha~~.
hii nayo nichangamoto inayo ikumba Tanzania.

Vinasa sauti, ~~nazo~~ hivi vyombo
vinaleta changamoto kubwa kwa wananchi
wa Tanzania kwa sababu inabagua baadhi
ya binadamu.

~~K~~ Uchanganyaji wa ~~tu~~ maneno ya
lugha mbili kwa wakati moja hii nayo ni
changamoto katika lugha ya kiswahili hapa nchi
ni Tanzania kwa mfano ~~ka~~ kuchanganya kiswah
ili na kingereza.

Hitimisho, japo kiswahili ina chang
amoto nyingi lakini ndo lugha nyepesitena
nzuri duniani.

Kielelezo 8.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika kama; *makosa ya kisarufi, utata katika sentensi, kutumia misimu, vinasa sauti na kuchanganya maneno ya lugha mbili*, mambo yasiyohusiana kabisa na changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili.

2.5.2 Swali la 9: Maendeleo ya Kiswahili

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* hususani katika mada ndogo ya *Changamoto za Kuenea kwa Kiswahili katika Afrika Mashariki kabla ya Uhuru* na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20 na lilimtaka mtahiniwa kufafanua sababu sita zilizochangia kutokukua na kutokuenea kwa lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa nchini Uganda kabla ya uhuru.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wachache (21.3%) ya watahiniwa wote kwani lilikuwa la kuchagua. Asilimia 92.8 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani kuanzia alama 12 hadi 19. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kiasilimia.



Chati Na. 7: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Zaidi ya nusu ya watahiniwa, (52.0%) walipata alama nzuri kuanzia 12 hadi 19, kwa kuwa walikuwa na maarifa kuhusu mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* na kuweza kufafanua kwa usahihi sababu zilizochangia lugha ya Kiswahili kushindwa kukua na kuenea kwa kiwango kikubwa nchini Uganda kabla ya uhuru. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 7.4 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kutokana na kuweza kufanua kwa mifano sababu za kutokukua na kutokuenea kwa Kiswahili nchini Uganda. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua kwa usahihi hoja kama; *lugha ya Kiswahili kuonekana kama lugha ya dini ya kiislamu, lugha ya kitumwa, kupata upinzani mkali kutoka katika lugha za kikabila na lugha ya Kiingereza, lugha ya Kiswahili kutotumika katika elimu, kutotumika katika utawala na kasumba kwa wasomi wanaodai kuwa*

lugha bora ni Kiingereza. Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu mazuri ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 9.1



9 Kukua kwa lugha ya kiswahili ni kuongezeka kwa msamiati wa kiswahili na kuenea kwa lugha ya kiswahili ni kuongezeka kwa watumiaji na mawanda yake katika matumizi. Uganda kabla ya uhuru ilikuwa chini ya utawala wa mwingereza ambapo lugha ya kiingereza ndiyo ilitumika zaidi kuliko lugha ya kiswahili.

Kifuatazo ni sababu zilizochangia lugha ya kiswahili isikue na kuenea kwa kiwango kikubwa nchini uganda kabla ya uhuru

lugha ya kiswahili kuonekana kama lugha ya dini ya kiislamu. Mchini uganda kabla ya ~~kiswahi~~ uhuru kilihusishwa kama lugha ya dini ya kiislamu ambayo ilikuwa inapingwa vikali na wamishenari wa dini ya kikristo nchini uganda na hivyo kukifanya kiswahili kushindwa kuenea uganda baada ya kukutana upinzani mkali kutoka katika dini ya kikrisao na lugha ya kiingereza na baganda kupewa kipaumbele.

lugha ya kiswahili ~~ka~~ ilionekana kama lugha ya kitumwa. Mchini uganda kabla ya uhuru lugha ya kiswahili ilitumiwa na polisi kuwatesa na kuwanyanyasa wananchi na hivyo kujulikana kama lugha ya kitumwa na wananchi kupendelea lugha yao itumika katika mawasiliano na shughuli za kila siku hivyo basi lugha ya kiswahili kukosa watumiaji.

Upinzani mkali kutoka katika lugha za kikabila na lugha ya kiingereza. lugha ya kiswahili nchini Uganda ilikumbana na changamoto ya kukosa watumiaji kwani lugha ya kiingereza na kiganda zilikuwa zimeshakwisha enea na hivyo wenyeji wa uganda kuona lugha yao ya kikabila ni bora zaidi kuliko kiswahili na kiganda kuweza kutumika katika shughuli zote za jami kabla ya uhuru.



9 Lugha ya Kiswahili kutotumika katika elimu. Kati
ka elimu nchini uganda lugha za kienyeji na kiinger
eza ~~kazi ka~~ zilitumika katika kufundishia kutoka shule za
msingi hadi elimu ya juu, wenyeji hawakupenda kutum
ia lugha ya kiswahili kwa kuona kuwa watashusha hadhi
ya lugha yao ya kikabili na hivyo kiswahili kukosa
watumiaji na kushindwa kukua na kuenea nchini ugan
da kabla ya uhuru.

Lugha ya Kiswahili kutotumika katika utawala.
wakati wa utawala wa waingerezi nchini uganda kiswahili
hakikupewa kipaumbele sana kitumika katika ngazi mbali
mbali za utawala ukilinganisha na lugha za kienyeji
na lugha ya kiingereza ambazo zilitumika katika uta
wala na hivyo basi kiswahili kushindwa kuenea nchini
uganda.

Kasumba. Lugha ya kiswahili ilionekana kama
lugha ya watu wa chini au duni na kutokana na hii kasu
mba wenyeji wakapendelea kutumia lugha yao ya ki
ganda na muda mwingine kiingereza na kukosekana k-
wa fursa ya kukua na kuenea kwa kiswahili nchini
uganda kabla ya uhuru.

Hivyo basi, lugha ya kiswahili ingeweza
kuenea kama ingetumika katika kufundishia elimu,
katika dini, utawala na matumizi ya kila sikuu

Kielelezo 9.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua vizuri sababu zilizochangia kutokukua na kutokuenea kwa lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa nchini Uganda kabla ya uhuru.

Watahiniwa wengine, (40.8%) walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kufafanua kwa usahihi baadhi ya sababu zilizochangia kutokukua na kutokuenea kwa lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa nchini Uganda kabla ya uhuru na kushindwa baadhi ya sababu nyingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua sababu nne kwa usahihi na kushindwa hoja mbili kwa kutoa hoja kama vile, *kuwepo kwa mbuga ya Tsavo nchini Uganda*, sababu ambayo si sahihi kulingana na matakwa ya swali. Kielelezo

9.2 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kutoa baadhi ya majibu sahihi na yasiyo sahihi.

Kielelezo 9.2



Kuwepo kwa mbuga ya Tsavo
hoi na mbuga ilyokuwa mpakani
Mwa Kenya na Uganda ndani
yake kulikuwa na wanyama
wakali sana. hivyo basi shugh
uli mbalimbali zilizokuwa zila
tumika pia na mchakato wa
kuenza kiswahili ulionokana
kuwa na tatizo kwa sababu
ukupita kabika mbuga hoyo unali
wa na wanyama hao kama
simba kwa hoyo kuenea kwake
kiswahili nchini humo ilikuwa
na tarabu sana ukilinganisha
na Kenya.

Kiswahili kutotumika katika
Elimu nchini Uganda kabla ya
uhuru. lugha ilyokuwa imatumika
na lugha za Makabila pamoja
na kiingereza. Kiswahili hawakuki
pa kipaumbele ili kifundishwe
Mashuleni hawa shule za msingi
Na hoi ni mojawapo ya sababu
zilizochangia lugha ya kiswahili isi
we na kuenea kwa kiwango kiku
bwa nchini Uganda.



Kielelezo 9.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kuelezea hoja ya *uwepo wa mbuga ya Tsavo* sababu isiyohusiana na kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda.

Hata hivyo, asilimia 7.2 ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa maarifa kuhusu historia ya kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda kabla ya uhuru. Wengi wao walitoa sababu zilizochangia kukua kwa lugha ya Kiswahili kama vile; *Kiswahili kutumika katika biashara, Kiswahili kama lugha ya taifa Uganda, kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli za kielimu na kiutawala* sababu ambazo hazina uhalisia kuhusu kutokukua na kutokuenea kwa Kiswahili nchini Uganda. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua sababu kama vile; *kukosekana kwa sera ya lugha ya Kiswahili, watangazaji mahiri wa Kiswahili, wataalamu, vitabu vya Kiswahili na kukosekana kwa*

vyama na taasisi za kukuza Kiswahili, sababu ambazo si sahihi. Kielelezo 9.3 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua sababu zisizo sahihi kuhusu kutokukua na kutokuenea kwa kiwango kikubwa kwa lugha ya Kiswahili nchini Uganda.

Kielelezo 9.3



9 Nchini Uganda kabla ya Uhuru, serikali ya
Uganda ilichukua baadhi ya hatua za kuzingatia
katika kukuza na kueneza lugha ya kiswahili
nchini humo baadhi ya hatua hizo zilizochukuliwa
ni kama; Kiswahili kiliweza kutumika katika shughuli
rasmi, pia katika mawasihano ya kibiashara,
kiswahili pia kiliweza kutumika kutolea Ilimu
hasa katika ngazi ya msingi.
Zifuatazo ni sababu zilizochangia lugha ya kiswahili
kisikue na kuenea kwa kiwango kikubwa nchini
Uganda kabla ya Uhuru'.
Hawakukithamini kiswahili, wananchi wa
Uganda hawakukithamini na kukipa kipaumbele
kiswahili kwani walikuwa na lugha zao za
makabila hivyo basi suala hili lilichangia
kuwepo kwa ari ndogo ya watu katika kujifunza
lugha hiyo.
Kukosekana kwa sera za kukuza na
kueneza lugha ya kiswahili nchini humo, pia
Uganda kulikosekana sera mbalimbali za kukuza
na kueneza lugha ya kiswahili ili iweze
kuenea na kufahamika sehemu nyingi zaidi
nchini humo. kwa kukosekana kwa sera hizo
kulipelekea lugha ya kiswahili isitihwe mkazo
nchini humo.
Kukosekana kwa watangazaji mahiri wa
lugha ya kiswahili, nchini Uganda, hasa katika
vyombo vya habari kama vile Redio, Runinga
na Magazeti hakukuwa na watangazaji mahiri
na waho bobea katika lugha ya kiswahili hivyo
kukifanya kiswahili kisijulikane, kisikue na kuenea
nchini humo kwa kari zaidi.



9 Ukosefu wa wataalamu, serikali ya Uganda ilikumbwa na tatizo la Ukosefu wa wataalam wa lugha ya kiswahili, kwani wahkuwa wakiazima wataalam kutoka Tanzania lakini bado serikali haikuweza kuwa na fedha nyingi za kuwalipa wataalamu hao. pia kuwa na ari ndogo ya watu kujifunza lugha hiyo kulipelekea wataalam wengi kushindwa kutamkisha zaezi hilo.

Ukosefu wa vitabu vya kiswahili, kabla ya Uhuru nchini Uganda, serikali ilikumbwa na tatizo la Ukosefu wa vitabu vya kiswahili ili viweze kutumika mashulem. Ukosefu huu ulipelekea serikali ya Uganda kutokipa kipaumbele kiswahili na kutiha mkazo katika lugha zao za ~~kig~~ makabila na lugha za kigeni.

Kukosekana kwa vyama na Taasisi za kukuza na kueneza lugha ya kiswahili, Nchini Uganda pia hakukuwa na Taasisi wala vyama vya kushughulikia Ukuaji na Uenezi wa lugha ya kiswahili nchini humo. Hivyo basi suala hili lilipelekea lugha ya kiswahili kulegalega bila ya kuwa na Usimamizi wowote.

Hivyobasi, Baada ya Uhuru nchini Uganda lugha ya kiswahili ilweza kutumika katika vyombo vya habari, pia katika shughuli za kisiasa pia serikali ilweza kuazima wataalam Mahiri na Wahotobea katika lugha ya kiswahili nchini Tanzania kwa lengo la kujifunza lugha hiyo kwa kina.

Kielelezo 9.3 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejadili matatizo yanayoikabili lugha ya Kiswahili baada ya uhuru badala ya kutoa sababu kutokukua na kutokuenea kwa lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa nchini Uganda kabla ya uhuru.

SEHEMU E: TAFSIRI NA UKALIMANI

2.5.3 Swali la 10: Tafsiri

Swali hili lilitoka katika mada ya *Tafsiri na Ukalimani* hususani katika mada ndogo ya *Tafsiri* na lililenga kupima tathmini ambapo lilikuwa na jumla ya alama 20. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja tano kuthibitisha kauli isemayo, "Katika Tanzania ya leo taaluma ya Tafsiri haiwezi kuepukika."

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali pekee katika sehemu hii. Asilimia 87.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya kufaulu kwa wanafunzi kiasilimia.



Chati Na. 8: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 51.9 ya watahiniwa walipata alama nzuri kuanzia 12 hadi 19, ambapo kati yao, asilimia 4.2 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kwa kuwa waliweza kutoa hoja tano kuthibitisha kauli isemayo; "Katika Tanzania ya leo taaluma ya tafsiri haiwezi kuepukika" na kuzitolea maelezo mazuri yaliyojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile; *maendeleo ya elimu yanahitaji tafsiri, wageni na watalii wanapokuja Tanzania kutoka sehemu mbalimbali duniani huhitaji tafsiri ili kuelewana na wenyeji wao, tafsiri huhitajika ili kurahisisha mawasiliano miongoni mwa watu wa lugha mbili tofauti, pia tafsiri ni nyenzo ya kujifunzia lugha ya pili*. Mtahiniwa huyo aliweza kutoa utangulizi

na hitimisho zuri linaloendana na swali. Kielelezo 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kukidhi matakwa ya swali.

Kielelezo 10.1

10 Tafsiri ni zoezi la uhamishaji
wa ujumbe kutoka lugha chanzi kuenda
lugha lengwa kwa nia ya maandishi.
Tafsiri inasaidia sana kueleza ujumbe ulopo
katika matini asilia kwani ujumbe na maw
aza katika matini chanzi huamishwa kama
yalivyo ili mkusanyaji wa lugha lengwa
aweze kuelewa kile kilichokusudiwa na matin
i chanzi. Kutokana na maendeleo mbalimbali
Tanzania kaeluma hii ya tafsiri haiwezi
kuepukika kwa sasa. Tafsiratoya ni mambo
yanayofanya taaluma ya tafsiri isiepukike
Tanzania ya leo.
Maendeleo ya Elimu; kutokana na
maendeleo ya Elimu, Tanzania imekuwa ikitaf
siri vitabu mbalimbali kutoka lugha za
kigeni ili kuweza kukidhi vyema uwanda
hilu wa elimu. Mfano katika shule za Sekon
dari, vitabu vingi vya hadithi vinavyo tumika
mfano "Orodha" vimetafasiriwa, pia kiswahili
usomwa hata katika ngazi za juu na
hii hupelekea hata wathanuzi kutoka Sehe
mu mbalimbali kuja ili wajifunze kiswahili.

10 Wageni na watalii wanaokuja Tanza
nia kutoka sehemu mbali mbali duniani;
watu hawa huja kwa lengo tofautitofauti,
kwani wengine huitaji kujifunza tamaduni
za waswahili, hivyo wanakuwa wanatafasiri
baadhi ya maneno ili waweze kuelewa japo
kidogo kuhusiana na mswahili.
Urahisi wa mawasiliano miongoni
mwa watu wa lugha mbili tofauti; Tafsiri
haiepukiki Tanzania kwani kutokana na
watu wanaokuja Tanzania kutoka sehemu
mbalimbali, tafsiri huwasaidia kupata
mawasiliano ya haraka. Hivyo wageni kawa
huweza kukaa Tanzania na kuwasiliana na
wengine kwasababu ya Tafsiri.
Maendeleo ya sayansi na teknolojia;
kutokana na maendeleo haya ya sayansi
na teknolojia, vitu vipya ugunduliwa na
hivyo vinapoingizwa nchini inabidi vitafasiri
we ili mswahili aweze kuelewa matumizi
na malengo yake. Mfano vitu kama simu,
Tanakilishi, kikokotozi na mengine mengine
yamekuja na kutafasiriwa kwasababu ya
maendeleo ya sayansi na teknolojia.
Ni nyenzo ya kujifunza lugha ya pili;
Hii ni kwasababu, kutokana na Tafsiri watanza
nia wengi huweza kujifunza lugha za
kigeni, ili waendapo nje waweze kuwasilia
na vyema na wageni. Mfano matumizi ya
"kamusi" yanasaidia kwa kiasi kiskubwa
kwa wanafunzi mashuleni na wasiokuwepo
mashuleni kujifunza lugha za kigeni kama

10 kiingereza ili waweze kukidhi vyema haja
ya mawasiliano na wenyeji wa lugha
hizo husika.
Hivyo kutokana na Tafsiri Tanzani
a imeweza hata kusaini mikataba mbali
mbali ili kudumisha umoja, mshikamano
na amani na nchi zingine ili kuweza
kuleta maendeleo Tanzania. Hivyo zoezi
hili la tafsiri haliwezi kuepukika kwa
sasa Tanzania.

Kielelezo 10.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyethibitisha kwa usahihi kauli isemayo; "Katika Tanzania ya leo, taaluma ya tafsiri haiwezi kuepukika na kupata alama za juu.

Hata hivyo, (35.3%) ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Hii ni kutokana na kuwa na maarifa kidogo kuhusu mada ya Tafsiri na kutoa baadhi ya hoja zilizo sahihi na nyingine zisizo sahihi katika kuthibitisha kauli isemayo, "Katika Tanzania ya leo taaluma ya tafsiri haiwezi kuepukika." Kwa mfano, katika kujibu swali hili, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile; *tafsiri hurahisisha mawasiliano, tafsiri wakati wa maendeleo ya sayansi na teknolojia na chanzo cha ajira* lakini hoja ya nne akaandika; *tafsiri haiwezi kuepukika kwa sababu ya kuwepo wamahiri wa lugha*; hoja ambayo si sahihi. Kielelezo 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyojitosheleza na kupata alama za wastani.

Kielelezo 10.2



10. Tafsiri ni kitendo cha
uhaulishaji wa ujumbe kutoka matini chanzi
kwenda matini lengwa kwa njia ya
maandishi. Ni dhahiri kwamba taaluma ya
tafsiri haiwezi kuepukika katika Tanzania
ya leo kutokana na sababu zifratazo.
Hurahisisha mawasiliano, taaluma
ya tafsiri haiwezi kuepukika kwani husaidia
katika kurahisisha mawasiliano baina ya
watu wawili wasiozungumza lugha moja.
mfano Mjerumani na mtanzania lazima ili
watu hawa waelewane taaluma ya tafsiri
itatumika tu. Hivyo ni vigumu kuepuka
taaluma hii katika Tanzania ya leo.
Maendeleo ya sayansi na
teknolojia, uwepo wa mabadiliko hasa
katika nyanja ya sayansi na teknolojia
yanachangia pia kukua kwa taaluma hii
ya tafsiri na kupelekea taaluma hii
kuzanyika hadi kwenye mitandao. Hivyo
inadhihirisha kwamba ni vigumu taaluma
hii kuepukika katika Tanzania ya leo.
Ni chanzo cha ajira, taaluma
ya tafsiri pia ni chanzo kikubwa cha
ajira miongoni mwa watanzania. Baadhi ya
watanzania hujishughulisha na taaluma ya
utafsiri wa kazi mbalimbali. Hivyo ni
vigumu kuepuka taaluma hii ndani ya
nchi ya Tanzania.
Umahiri wa lugha, taaluma
ya tafsiri haiwezi kuepukwa kutokana
na uwepo wa watu ambao ni wamahiri


10. wa lugha zaidi ya moja. Ambao hawa
ndio hujishughulisha na masuala ya utafsiri
Hivyo kutokana na uwepo wa wamahiri wa
lugha zaidi ya moja ni rigumu kuepuka
taaluma hii dhani ya Tanzania.
Kiujumla taaluma ya tafsiri
haiweri kuepukika katika Tanzania yaleo
licha ya kuwa inakumbwa na matatizo
mbalimbali kama vile athari za lugha mama
na uhaba wa wamahiri wa lugha.

Kielelezo 10.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa majibu matatu sahihi, moja lisilo sahihi na kushindwa kumalizia hoja ya tano.

Aidha, asilimia 12.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Tafsiri na hivyo kushindwa kuthibitisha kauli isemayo, "Katika Tanzania ya leo taaluma ya tafsiri haiwezi kuepukika" kwa kutoa hoja zisizohusiana kabisa na umuhimu wa tafsiri. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama; *uwepo wa nadharia mbalimbali, isimu linganishi, semantiki, mantiki, falsafa na kuhakiki matini*, hoja ambazo hazihusiani kabisa na umuhimu wa tafsiri na hivyo kupata 0. Kielelezo 10.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua mambo yasiyohusu umuhimu wa taaluma ya tafsiri katika Tanzania ya leo .

Kielelezo 10.3



10. Ni kweli kwamba katika Tanzania ya leo taaluma ya tafsiri haiwezi kuepukika. Taaluma ya tafsiri ni yale ma funzo au maelezo anayo yapata Mfasiri ili kumsaidia wakati wa kufanya zoezi la kutafsiri Matini fulani au kifungu fulani cha Habari. Dai hili la kuwa Nadhalia ya tafsiri haiepukiki ni kweli hi yo ni kutokana na kuwepo nadhalia mbalimbali za Tafsiri. Kama ifuatavyo:

Isimu Linganishi; Hii ni taaluma inayo jihusisha na Ulinganishaji wa vipengele Mbalimbali vya Lugha zaidi ya Moja. Kwa hivyo basi ~~vipen~~ kuwepo kwa taaluma kama hii ya isimu Linganishi kunawezo kumsaidia Mfasiri kujua vipengele mbalimbali vya Lugha zaidi ya moja Mfano, Maana, ~~Maana~~ Matamshi, Miundo na maumbo mbalimbali ya Lugha...

Semantiki; Hii ni taaluma inayo jihusisha na maana. Kuwepo kwa taaluma hii kunamsaidia Mfasiri kujua Maana za maneno mbalimbali na Tungo. Hivyo basi kuwepo kwa taaluma hii ya semantiki kunafanya taaluma ~~ya~~ tafsiri isiepukike.

Mantiki; Hii hujihusisha na mtiririko Mzuri wa Mawazo. Taaluma hii ya mantiki humsaidi Mfasiri kujua ukweli wa kauli mbalimbali, Hasa pale anapofanya zoezi lake la kufasiri. Kwa hivyo basi taaluma hii pia inafanya taaluma ya tafsiri isiwezo kuepukika.

Falsafa; Falsafa pia ni Miongoni mwa taaluma za tafsiri na ukalimani. Taaluma hii hujihusisha na kusisitiza kufuata Maana za maneno mbalimbali yaliyopo katika Lugha kulingana na Muktadha wa Matamiti yake. Kwa hivyo kuwepo kwa nadhalia hii ya Falsafa imefanya taaluma ya tafsiri isiepukike.

Kuhakiki Matini; Pia taaluma hii hujihusisha na kuhakiki matini au ni taaluma inayo jihusisha na kuhakiki matini kabla ya kuanza kuifasiri au baada ya kuifasiri. Taaluma husaidia kutolewa fusili nzuri na inayo eleweka na Mfasiri.

10 Hivyo basi inapaswa wafasiri wengi au kwanao jihusisha na zoezi la kutafsiri ni vyema wajue vyema taratibu hizi au taaluma hizi ili kuwasaidia ~~kutoa~~ kutoa Tafsiri zinazo eleweka kwa wasomaji lengwa ya ani Hadhira ifaswa

Kielelezo 10.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama 0 kwa kutoa hoja zilizo kinyume na matakwa ya swali.

3.0 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI

3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI

3.2 SEHEMU A: FASIHI KWA UJUMLA

3.2.1 Swali la 1: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla* na lilihusu Fasihi Simulizi na lilikuwa na jumla ya alama 20. Swali lililenga kupima tathmini na lilimtaka mtahiniwa kutumia mifano kueleza hoja nne zinazodhihirisha uhai wa fasihi simulizi na hoja mbili kudhihirisha uhalisia wa fasihi simulizi kwa jamii dhidi ya fasihi andishi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 15,332 sawa na asilimia 75.1 ya wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali la kuchagua. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo asilimia 69.5 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na. 3 linaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.

Jedwali Na. 3: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Watahiniwa	Asilimia ya Watahiniwa
0.0 - 6.5	4670	30.5
7.0 - 11.5	7670	50.0
12.0 - 20.0	2992	19.5

Asilimia 50.0 ya watahiniwa yaani nusu ya wote waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Watahiniwa hao waliweza kueleza baadhi ya hoja zinazodhihirisha uhai na uhalisia wa fasihi simulizi kwa jamii dhidi ya fasihi andishi kwa usahihi, japokuwa walishindwa kutoa maelezo toshelevu kwa baadhi ya hoja na kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kudhihirisha uhai wa fasihi simulizi alitoa hoja tatu sahihi kama vile: *fanani na hadhira huonana; huwa na ushirikishwaji na huwa na utendaji*. Pia, mtahiniwa huyo alitoa hoja moja isiyo sahihi kwa kueleza kuwa, *hutumia mazungumzo ya mdomo* hoja ambayo si sahihi. Adha, katika kudhihirisha uhalisia wa fasihi simulizi kwa jamii, mtahiniwa alitoa hoja mbili zisizokidhi matakwa ya swali kama vile; *hadithi za sungura na fisi* na *vitendawili* bila kuhusisha

uhalisia uliopo katika utendaji wa tanzu hizo kwa jamii. Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kutoa maelezo yasiyojitosheleza kwa baadhi ya hoja.

Kielelezo 1.1



1 Fasihi Simulizi. Ni aina ya fasihi ambayo hutu
mia mdomo au mazungumzo katika Utikishaji ujumbe
katika jamii husika. fasihi Simulizi hutumia njia ya
mdomo au maongezi kutikisha Ujumbe wake kwa
jamii mfano hadithi, Vifendawili, Ngonjera
Zifuatazo ni hoja zinazodhihirisha Uhai wa fasihi
Simulizi katika jamii
Hutumia Mazungumzo ya mdomo, Ni moja ya
mambo yanayothihirisha Uhai wa fasihi simulizi kwa
sababu hutumia mdomo kutoa Ujumbe mbalimbali
Kama vile masimulizi ya hadithi pia tunaona fa
sihi ya simulizi Uhai wake pale watu wawili
wanapo zungumzo pamoja na kuelewana pia huu
ni Udhibitisho kwamba fasihi simulizi Iko hai
Fanani na hadhira huonana, pia nimiongoni
mwa mambo yanayothihirisha Uhai wa fasihi
simulizi kwa sababu fanani na hadhira huonana
yaani msimuliaji na wasimuliwaji huonana ana
kwa ana tofauti kubisa na fasihi andishi
ambapo wahusika hawa onani kutokana na
kuonana kwa fanani na hadhira huonyesha dhahiri
Uhai wa fasihi simulizi katika jamii sefa zakuku
Huwa na Ufendaji, Ni miongoni mwa mam
bo yanayo onesha Uhai wa fasihi simulizi
kwa sababu huwa na Ufendaji mfano msimuli
aji huweza kucheza, kuonyesha Ishara za
mikono kama Sungura akaenda akaenda huonye
sha Ufendaji mbalimbali kama kutikisa kichwa
kwaiyo fasihi simulizi huonyesha Uhai wake
katika Ufendaji wa mambo kadha wa kadha
katika Utikishaji wake Ujumbe katika jamii



Kielelezo 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja zisizojitosheleza katika kudhihirisha uhai na uhalisia wa fasihi simulizi kwa jamii dhidi ya fasihi andishi.

Aidha, watahiniwa wachache, asilimia 19.5 walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia 12 hadi 19. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu *uhai* na *uhalisia* wa fasihi simulizi kwa jamii na kuweza kuelezea hoja nne sahihi kuhusu uhai wa fasihi simulizi na hoja mbili kuhusu uhalisia wa fasihi simulizi zikiambatana na mifano iliyokidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja nne zinazoelezea uhai wa fasihi simulizi kwa jamii dhidi ya fasihi andishi kama vile; *uhusiano baina ya fanani na hadhira, huweza kubadilika kulingana na wakati au mazingira, huwa na tendaji, huwa na mandhari au uwanja wa kutendea*; na kiuhalisia, mtahiniwa huyo alielezea kuwa fasihi simulizi ni *mali ya jamii nzima, huzaliwa, hukua au hustawi na*

kufa. Aidha, mtahiniwa huyo alitoa utangulizi na hitimisho zuri linaloendana na matakwa ya swali. Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja nne kwa usahihi katika kudhihirisha uhai wa fasihi simulizi na hoja mbili kudhihirisha uhalisia wa fasihi simulizi kwa jamii dhidi ya fasihi andishi.

Kielelezo 1.2

1. Fasihi simulizi ni aina ya fasihi ambayo huwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Aina hizi ya fasihi zna tanzu mbalimbali ambazo ni Hadithi, Ushairi, Semi na Sanaa za maonyesho.

Fasihi andishi ni aina ya fasihi ambayo huwasilishwa kwa njia ya maandishi. Aina hii ya fasihi pia zna tanzu mbalimbali ambazo ni riwaya, tamthiliya na Ushairi. Fasihi simulizi ni kongwe sana kuliko fasihi andishi kwa sababu ilianza tangu enzi za mababu zetu na fasihi andishi ilianza mara baada ya kugundulwa kwa maandishi. Pia fasihi simulizi ni hai na halisi kuliko fasihi andishi.

Zifuatazo ni hoja zinazodhihirisha uhai wa fasihi simulizi.

Uhusiano baina ya fanani na hadhira; katika fasihi simulizi fanani na hadhira huweza kuonana na kushiriki mambo mbalimbali kwa pamoja. Mfano kuimba na kupiga makofi tofauti na fasihi andishi ambapo mwandishi haweri kuonana na msomaji.

Hubadilika kulingana na wakati na mazingira; Pia fasihi simulizi ni hai kuliko fasihi andishi kwa sababu huweza kubadilika kulingana na wakati na mazingira. kwa mfano katika masimulizi ya hadithi fanani anaweza kutaja na hadhira wanawe za kumrekebisha.

Utendaji; Pia uhai muingine wa fasihi simulizi unajidhihirisha katika utendaji. kwa mfano, vitendo mbali mbali vinaweza kujitokeza katika fasihi simulizi kama kucheza, kuimba, kuruka au kupiga makofi tofauti na fasihi andishi ambapo mwandishi huandika kazi yake na kuwachia wasomaji wasome bila utendaji wa aina yoyote.



1. Mandhari au uwanja wa kutendeq; katika fasihi simulizi, mandhari yake huwa ni halisi sana na inayoonekana kuliko ilivyo kwa fasihi andishi. Mfano, yanaweza kuwa mandhari ya shuleni, nyumbani, chumbani au barabarani ambayo huambatana na utendaji wa vitendo mbalimbali.

Zifuatazo ni hoja zinazodhihirisha uhalisia wa fasihi simulizi.

Fasihi simulizi ni mali ya jamii nzima; hii ina maana kwamba fasihi simulizi humilikiwa na watu wote wanaojua kusoma na kuandika na wale wasiojua kusoma na kuandika, lakini fasihi andishi yenyewe ni mali ya watu wachache katika jamii wale wanaojua kusoma na kuandika peke yao.

Fasihi simulizi huzaliwa, hukua, hustawi na kufa; pia uhalisia mwingine wa fasihi simulizi ni kwamba inazaliwa, inakua pia inakufa. kwa mfano zipo fasihi simulizi mbalimbali kama hadithi au sanaa za maonyesho ambazo zilianza tangu enzi za mababu zetu, zilikua na hatimaye zikafa na zikazaliwa zingine.

Jumla; Ingawa fasihi simulizi ni hai na halisi kuliko fasihi andishi, aina hizi za fasihi zina umuhimu na dhima zinazofanana katika jamii zetu. kwa mfano, kuelimisha jamii, kuburudisha jamii, kuonya jamii, kutunza na kurithisha amali za jamii, kuliwaza jamii pia kukuza na kuendeleza lugha.

Kielelezo 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja sahihi zinazodhihirisha uhai na uhalisia wa fasihi simulizi kwa jamii dhidi ya fasihi andishi.

Hata hivyo, asilimia 30.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifanya vibaya kwa kupata alama za chini kuanzia 0 hadi 6. Hii inaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na uelewa mdogo kuhusu dhana ya uhai na uhalisia wa fasihi simulizi kwa jamii na jinsi zinavyodhihirishwa katika uwasilishaji wake. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile; *suala la kuchanganya mapenzi na kazi*, *umaskini*, *rushwa*, *ulevi* na *dhuluma*; hoja ambazo zilikuwa kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 1.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja zisizodhihirisha uhai na uhalisia wa fasihi simulizi kwa jamii dhidi ya fasihi andishi kwa kuandika

dhamira mbalimbali zinazopatikana katika vitabu vya kifasihi kinyume na matakwa ya swali.

Kielelezo 1.3

1 Fasihi simulizi ni aina ya fasihi inayowalishwa kwa nzia ya masimulizi ya mdomo kuna vipera mbalimbali vya fasihi simulizi pamoja na hadithi, semi, ushairi na sanaa za maonyesho. Fasihi simulizi ni hai na halisi zaidi ya fasihi andishi na pia zinadhihirisha uhalisia wa fasihi simulizi kwa jamii. Hivyo basi fasihi simulizi zina uhai ni hai hivyo hoja zifuatazo zinaonyesha uhai wa fasihi simulizi

Suala la kuchanganya mapenzi na kazi hii inajidhihirisha kuwa fasihi ni hai kwani maanii ameonyesha hili katika tamthiliya ya ngoswe penzi kitovu cha uzembe alivyochanganya mapenzi kwa kuangukia katika penzi la mazoea na kuharibu kazi yake iliyompeleka hivyo fasihi ni hai kwani maanii ameweza kuonyesha vitu ambavyo vinapanyika katika jamii yetu.

Umaskini hii inajidhihirisha kuwa fasihi ni hai kwani maanii ameonyesha hili katika Fdhaaya ya watoto wa mama ntilie " umaskini, familia inayoishi na dhiki watoto wanakosa sare za shule wanaenda shuleni peku peku hivyo basi fasihi simulizi ni hai kwa sababu zinaonyesha mambo yanayotokea katika jamii yetu

Rushwa: hii inajidhihirisha kuwa fasihi ni hai kwani maanii ameonyesha hili katika riwaya ya joka la mdimu jinsi Boaz alipokuwa anapokea rushwa jambo ambalo hata katika jamii yetu ya kila siku wapo wanaopokea rushwa kwa ajili ya kufanikisha jambo fulani hivyo fasihi simulizi ni hai na halisi

Suala la ulevi, wizi na ujambazi hii inajidhihirisha kuwa fasihi ni hai kwani maanii ameonyesha katika riwaya la watoto wa mama ntilie jinsi watoto hawa maskini walivyojiingiza kahka ulevi, wizi na ujambazi mpaka na umauti kuwakuta hivyo maanii ameonyesha

1 mamba yanayotokea pia katika jamii yetu kuna watu wanaojiingiza katika modewa ya kulevya, wizi na ujambazi ili kuweza kupata pesha ili kuendeleza maisha yao hivyo basi fasihi simulizi ni hai na halisi zaidi Zipuatazo zinagidhihirisha uhalisia wa fasihi simulizi kwa jamii

Mapenzi, suala la mapenzi linaonyesha uhalisia kwa jamii zetu katika hadithi na riwaya zinatupundisha na zina dhamira ya mapenzi hivyo katika jamii zetu hili linaonyesha kuwa kuna jamii wanaishi kwa upendo, kupendana hivyo fasihi simulizi zinaonyesha uhalisia kwa jamii

dhuluma, pia dhuluma inadhihirisha uhalisia katika fasihi simulizi mfano hadithi ya Jongoo na nyoka inaonyesha Jinsi nyoka alivyomdhulumu macho yake Jongoo kwani yeye aliomba kwa ajili ya kwenda tu kwenye tafiJa alafu amrudishie hivyo Fasihi simulizi zinadhihirisha pia katika jamii zetu kuna jinsi watu wanavyodhulumiwa mali zao hivyo hii inaonyesha uhalisia.

Hitimisho: basi fasihisimulizi ni hai na halisi zaidi ya fasihi andishi kwani zinatumika kutupa dhamira mbalimbali na mafunzo yatokanayo katika jamii zetu siku zote.

Kielelezo 1.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua dhamira mbalimbali kutoka katika riwaya ya ‘Mama N’tilie’ na ‘Joka la Mdimu’ badala ya kudhihirisha *uhai* na *uhalisia* wa fasihi simulizi kwa jamii dhidi ya fasihi andishi kupitia sifa za fasihi simulizi.

3.2.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla* hususani mada ndogo ya *Matambiko.* Swali lililenga kupima maarifa ambapo mtahiniwa alitakiwa kufafanua dhima nne za matambiko katika jamii enzi za mababu zetu na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Watahiniwa wachache, asilimia 24.1 ndio waliojibu swali hili kwa kuwa lilikuwa la kuchagua. Swali lilijibiwa vizuri ambapo asilimia 63.4 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na. 4 linaonesha viwango vya watahiniwa vya kufaulu kwa asilimia.

Jedwali Na. 4: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Watahiniwa	Asilimia ya Watahiniwa
0.0 - 6.5	1804	36.6
7.0 - 11.5	2043	41.4
12.0 - 20.0	1082	22

Takwimu zinaonesha kuwa, asilimia 41.4 ya watahiniwa walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kufafanua baadhi ya dhima za matambiko zisizojitosheleza. Kiwango hiki cha kufaulu kinaonesha bayana kuwa, watahiniwa wengi hawakuwa na maarifa toshelevu kuhusu dhima za utanzu wa matambiko enzi za babu zetu kama vile; *kuomba miungu/mizimu dhidi ya majanga ya asili*, *kuomba hekima na heshima kwa miungu*, *kuomba radhi au kutoa shukrani kwa miungu kwa mafanikio mbalimbali*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua hoja kama, *"kuomba kuondolewa laana, kuomba kupata mtoto, kuomba mvua*; hoja ambazo kimsingi zinafanana na hivyo kuwa na hoja pungufu na kupata alama za wastani. Hata hivyo, mtahiniwa huyo aliweza kufafanua hoja sahihi kama vile; *kutoa shukrani kwa miungu yao baada ya kuwatendea vile walivyotarajia*. Aidha, aliweza kutoa utangulizi na hitimisho zuri lililoakisi dhima za matambiko katika jamii enzi za mababu zetu. Kielelezo 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 2.1

2. Matambiko, Ni moja wapo ya utamu
wa ~~[illegible]~~ ~~[illegible]~~ hadithi ambao umekuwa
ukitumiwa na watu wa kale kuabudu
mungu wao. Ambapo mara nyingi matambiko
hayo yamekuwa yakifanyika katika malezo
maalumu mfano chini ya miti mikubwa kama
mbuyu, Nyika panda na katika mapango
makubwa ya mawe. Mara nyingi yamekuwa
yakifanya na koo ambazo zinafata mila na
desturi za koo zao. Zifuatazo ni dhima za
za matambiko kwa jamii wakati huo;-
Kuomba kuondolewa laana na mikosi
katika familia au jamii zao ambapo sadaka
mbalimbali zimekuwa zikitolewa ili kuwao-
mba mungu wao wawaepushe na laana, mikosi
na kila aina ya mabalaa ambayo yamatoke
a au ya sitarajia kutokea katika jamii zao
Kutoa shukrani kwa mungu yao
baada ya kuwatendea kama vile walivyo



2. walivyo tafsiri. Ambapo sadaka mbalimbali
na bafuta za wanyama, ndege na vitu vingine
zilitolewa ili kuwatizisha miungu wao.
Kuomba kupata mtoto kwa familia ambazo
zilikuwa zinahitaji watoto. Ambapo watu wali-
fanya matambiko hayo kwa kuomba kwa
Miungu wao kuwapatia kupata watoto na
pia walimia kama njia moja wapo ya kuwasili-
ana na mungu wao pia ya matatizo yao
mengine.
Kuomba mvua na kujaliwa mazao mengi
ili lilifanywa zaidi na watu wa kimila ambapo
baada ya kulima waliomba mvua kwa mungu
wao ili wapate kuzalisha mazao mengi pia
waliomba mvua kutokana na tatizo la
kukosa mvua kwa muda mrefu. Hivyo wali-
fanya matambiko ili kuomba kwa mungu
wao pia sadaka mbalimbali zilitolewa.
Hivyo basi, Matambiko yalikuwa na
umuhimu mkubwa kwa jamii za wakati
huo lakini kutokana na maendeleo ya sayansi
na teknolojia jamii za sasa hazifuati
tena matambiko hivyo imesababisha baadhi
ya mila na desturi za watu kuwahawiba.

Kielelezo 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa yasiyojitosheleza kulingana na matakwa ya swali na kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa wachache, asilimia 22.0 walijibu swali hili vizuri na kupata alama kuanzia 12 hadi 19. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa mahsusi kuhusu dhima za matambiko kwa jamii enzi za mababu zetu. Miongoni mwao, watahiniwa wachache, asilimia 1.7 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kutokana na kukidhi matakwa ya swali kwa kiwango cha juu. Watahiniwa hao walitoa kwa usahihi dhima za matambiko katika jamii kama vile; *Kuomba mvua na mavuno mazuri, kuomba ili*

kuepukana na magonjwa au matatizo mbalimbali, kuwaombea watu msamaha kulingana na makosa waliyoyafanya na kwa ajili ya kumshukuru Mungu kwa kuwatimizia haja zao za kimaisha. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili japokuwa alikuwa na tatizo la kitahijia kwa baadhi ya maneno kama alivyoandika “kumshuru mungu” badala ya “kumshukuru Mungu.”

Kielelezo 2.2



02. Matambiko; Ni ibada amba walizita
mia wata wa zamani au wazee wata wa za-
mani katika swala la kuomba mambo ambayo
walikuwa wanayahitaji kwa kipindi maalumu
ambacho wakuwa na mahitaji haya kwa mfan-
o maombi ya muwa, mauwano
Zifuatazo ni shima za matambiko
katika jamii ya wata wazani.
Kuomba muwa au mauwano mazuri ya
mazao; Moja ya sima ya kufanya matambi
ko kwa wazee wa zani ni kwaili ya kuomb-
a muwa kipindi cha ukame au kipindi cha jua
kali ili wapate mauwano yaliyo mazuri na
kukidhi mahitaji yao c'ya Chakula kwa ajili
ya jamii nzima
Kuomba ili waepukane na maj-
anga au matatizo mbalimbali kama vile uk-
ame au jenga la njaa; Pia wata wa zamani
walikikuwa wakifanya matambiko ili kuepuk-
ana sharuba mbalimbali ambazo zinatoke kupa
alimwungu ni kama njaa, kiangazi kikali
Pia matambiko yalifanyaa kwa
shamira ya kuwaombea watu msamaha
kulingana makosa waliyoyafanya; Hiyohiyo
o matambiko yalikuwa yanafanyika kwa lengo
la watu kuombeaa msama ~~m~~ kwa mungu
ili wapate kusamaha shambi zao na mungu
ili wapate maisha yaliyo mazuri na yenye
amani
Pia matambiko yalifanyika kwa
shima ya ~~kumsh~~ kumshuru mungu kwa
a kuwatimizia haya zao za kimaisha; Pia



Kielelezo 2.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua vizuri dhima nne za matambiko kwa jamii enzi za mababu zetu.

Kwa upande mwingine, asilimia 36.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 6.5. Kati yao, watahiniwa wachache (45) sawa na asilimia 0.3 walipata alama 0 kwa kuwa walishindwa kufafanua dhima hata moja kuhusu matambiko kwa kuwa hawakuwa na maarifa mahsusi kuhusu lengo la matambiko enzi za mababu zetu. Katika kujibu swali hili, baadhi ya watahiniwa walielezea; *tofauti kati ya fasihi simulizi na matambiko*, *sifa za fasihi simulizi*, *dhima za fasihi simulizi* na dhana nyingine za kifasihi zisizokidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua dhima za fasihi simulizi kama vile; *kuelimisha jamii; kutunza na kuhifadhi historia ya jamii; kukuza lugha na kuburudisha jamii*, badala ya kufafanua dhima za matambiko. Kielelezo 2.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua dhima za matambiko enzi za mababu zetu na kupata alama 0.

Kielelezo 2.3

2 Matambiko ni ama za ~~hadithi~~ mechezo ambazo
zilikuwa ~~zikisimuliwa~~ zikichezwa na babu zetu walio
pita. Kupitia tambiko hizo kuna dhima
mbali mbali ambazo zilikuwa zenapatikana
kupitia tambiko hilo miongoni mwa dhima
hizo ni kama zifuatazo:
Kwanza, kuelimisha jamii: Jamii ilipata
kuelimika kupitia tambiko kwa kuelezea
yale mambo halisi janayofanyika kwa
mfano tambiko hizo zilikuwa zenaelezea
masuala la ulua, ubakaji na mengineyo.
Kutunza na kuhifadhi historia ya jamii.
Babu zetu walitwekewa historia ya kujua
kama zama zao walikuwa na mechezo ya
tambiko kupitia mechezo hijo kuna misa
miato ambayo walikuwa wanaetumia na

2 sisi tukaweza kuifahamu katika jamii zetu.
Kukuza lugha: lugha hukua kutokana
na kutumiwa katika shughuli mbali mba
li kwa hijo kutokana na kuwa tambiko
ni miongoni mwa shughuli ambazo zilikuwa
zikifanywa lugha ikapelekea kukua.
Kuburudisha jamii: Kupitia tambiko
watu huburudika kutokana ratuko mbali
mbali ambazo zanafanywa na wachezaji hao
kwa kuonesha ratendo au kwa ujia joyote.
Kwa hijo kutokana na kuwa tambiko
lilikuwa likichezwa na babu zetu ndo ika
pelekea hadi leo tunapata matunda mbali
mbali kupitia tambiko.

Kielelezo 2.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua dhima za fasihi simulizi kwa jamii kutokana na kukosa maarifa mahsusi kuhusu dhima za matambiko katika jamii enzi za mababu zetu.

3.3 SEHEMU B: USHAIRI

3.3.1 Swali la 3: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* na lilihusu uhakiki wa vitabu teule vya ushairi. Swali hili lililenga kupima uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kauli "Msanii wa ushairi ni tabibu wa magonjwa sugu yaliyopo kwenye jamii" kwa kutoa hoja nne kwa kila diwani kutoka katika vitabu viwili vya ushairi alivyosoma na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na zaidi ya nusu ya watahiniwa yaani asilimia 57.6 kati ya wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali la kuchagua. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana na watahiniwa wengi kwani asilimia 99.4 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na. 5 linaonesha asilimia za viwango vya kufaulu kwa watahiniwa.

Jedwali Na. 5: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Watahiniwa	Asilimia ya Watahiniwa
0.0 - 6.5	67	0.6
7.0 - 11.5	668	5.7
12.0 - 20.0	11020	93.7

Swali hili liljibiwa vizuri sana kwani watahiniwa wengi, asilimia 93.7 walifaulu vizuri kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 19 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mawazo makuu ya washairi katika diwani mbili teule walizozisoma. Miongoni mwao, asilimia 29.5 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kwa kuwa waliweza kuthibitisha kauli inayosema, "Msanii wa ushairi ni tabibu wa magonjwa sugu yaliyopo kwenye jamii" kwa kutoa hoja na mifano sahihi ya mashairi kutoka diwani husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia diwani ya "Chungu Tamu" na kutoa hoja kama vile; *kupiga vita dhuluma, uongozi mbaya, mapenzi ya uongo na matabaka* huku akitoa ufafanuzi kwa kutumia mashairi yaliyoakisi dhamira hizo. Aidha, katika diwani ya "Kimbunga" alitoa hoja kama vile; *kupiga vita suala la usaliti, unyonyaji, umbea na rushwa* na kutoa mifano sahihi ya mashairi kutoka katika diwani hiyo ili kushadidia hoja zake kama ilivyotakiwa. Kielelezo 3.1 ni

sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri na kupata alama za juu.

Kielelezo 3.1

3. Msanii, Ni mtu anayetumia mela
wake mwingi kuzungumza na jamii
yake ili kutoa mafunzo. Msanii wa Mshairi
ni tabibu wa Magonjwa sugu kupitia
diwani ya CHUNGU TAMU ya Theobald
Mrungi na KIMBUNGA ya Haji Gora
wameonesha utabibu wa Msanii wa
~~Msha~~ Mshairi katika kutibu magonjwa
yanayo isumbua jamii yake.
Kwanza, katika diwani ya CHUNGU
TAMU Theobald ameonesha utabibu
wake kwa kupinga Maovu yote kati
ka jamii ili watu wapone kama
ifuatavyo:
Kupiga vita suala la dhuluma, Msanii
wa Chungu tamu ameonesha dhuluma
kama moja ya gonjwa sugu kwa jamii
na Msanii Theobald anasisitiza kupiga
vita suala hili. hii inadhihirishwa
katika shairi la CHATU NA KUKU
Msanii anasema
"Siku zikapita,
Adha imempata,
Japo kwa woga,
Mayai akaya taga,
Chatu waka yameza,
Wakamsifu paku kwa kum
beza".
hiryo Msanii Theobald anasisitiza suala
la kupiga vita dhuluma ikiwa kama
dawa yake, hata katika jamii zetu
watu washikamane kupiga vita suala hili.

3. Kupiga vita suala la Uongozi mbaya, Msanii anatoa njia ya kutibu gonjwa la Uongozi mbaya ili viongozi wanaochaguliwa wawe wakweli, wazwazi na wafuate demokrasia. hii imedhihirika katika shairi la TISHIO LA BINADAMU Msanii anaposema

"Mashindano ya silaha yamekua ni Mchezo,
Wakubwa waona raha kwa silaha waundazo,
Mabomu yaso nasaha ndio yawapa uwezo,
Urusi na Marekani dunia Mwapa adha".

Pia katika jamii zaleo ni lazima kupinga Uongozi mbaya ili jamii ipate Maendeleo bora na imara.

Kupiga vita suala la Mapenzi ya Uongo, Msanii anatibu suala la Uongo katika mapenzi maana ni chanzo cha migogoro na kurudisha nyuma Maendeleo. hii inadhihirika katika shairi la FIKIRA ZA WAUNGWANA Msanii anaposema

"Mume wangu nakupenda joseph kani kuna
Nimekula nae tunda nilipenda sana,
Nitaishi kwa mpango kwako na
kwa joseph".

Pia katika jamii zetu wapo wanawake ambao hawaridhiki na waume zao ndio Maana Msanii Theobald anatibu gonjwa hili ili wanawake wapate elimu na wawapende waume zao

Kupiga vita suala la Matabaka, Msanii ametibu suala la matabaka maana huleta utengano katika jamii na-



3. hukwamisha Maendeleo ya jamii kwa
ujumla hii imedhihirika katika
Mashairi kama vile MANZESE MPAKA
OSTABEI, CHATU NA KUKU na THOMAS
NA DOTTO. Ambapo Msanii ~~anes~~
katika shairi la THOMAS NA DOTTO
anasema

"Thomas umelaanika,
Wazuri ni wa landani,
Weusi hawaja kufaa,
Utaharibu wako ubwana".

Pia katika jamii zetu matabaka huto
kea hasa kwa tabaka tawala na tawali
wa na tabaka la wenyenacho na wasiona-
cho ndio Maana Mwandishi ~~ata~~ anaa
mua kutibu suala hili.

Pili, katika diwani ya KIMBUNGA
Haji Gora amedhihirisha utabibu wake
kwa kupinga magonjwa au Mauvu yote
katika jamii kama ifuatavyo:

Kupiga vita suala la Usaliti, Msanii
ameonesha usaliti ni moja yagonjwa lina-
loitesa jamii Maana hurudisha Maendele-
onyuma. amedhihirisha katika shairi
la KIMBWANGAI anaposema

"Kimbwangai liipoona,
Ni mtu, binadamu kukamiliya,
Akaanza kujivuna,
Akasahau yu nyani asilia".

Mambo ya usaliti hutokea kwa jamii
za leo na kuleta migogoro mingi sana

Kielelezo 3.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyethibitisha kwa usahihi kauli inayosema “Msanii wa ushairi ni tabibu wa magonjwa sugu yaliyopo kwenye jamii” kwa kutumia diwani ya “Chungu Tamu” na “Kimbunga”.

Hata hivyo, asilimia ndogo ya watahiniwa (5.7%) waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa baadhi ya hoja ambazo maelezo yake hayakujitosheleza kuthibitisha kauli isemayo, “Msanii wa ushairi ni tabibu wa magonjwa sugu yaliyopo katika jamii.” Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa baadhi

ya hoja zisizojitosheleza kama vile; hoja ya kwanza katika diwani ya “Kimbunga” aliandika maelezo yasiyoeleweka kama; *ni vizuri kupokea na kutoa rushwa kwenye jamii kwa sababu huchangia kupotea kwa haki na usawa wa watu*, pia katika diwani ya “Chungu Tamu” katika hoja ya kwanza, hakutoa ufafanuzi unaojitosheleza kuhusu shairi la *Chatu na Kuku* ili kuelezea hoja yake ya *matabaka.*

Kielelezo 3.2



3. Msanii ni Mtu ambaye huweza Kufikisha
ujumbe kwa jamii yake iliyokusudiwa kwa kuweza
au Kufanikiwa Kuhakisi na Kufundisha pameja na
yale Matatizo yale ambayo yanajitokeza kwenye
jamii yetu. Pia kwa upende wa Msanii ni mtu
ambaye huweza kuibua jambo jipya ambalo ni
Moja ye Mabadiliko kwenye jamii. Kwa kufumia
diwani ya "Kimbunga" na "Chungu tamu"
ambaye inaweza onesha Msanii wa Ushairi kuwa ni
tabibu wa Magoniwa tugu. Kwa kwanza na diwani ya "Kimbunga"

3- Msanii amepiga Vita Suala la Wizi na udokozi. Pia kupitia Wizi na udokozi ni dai ambazo Mwandishi amezizungumzia katika Shairi la "Paka" Msanii ameweza kuonyesha tatizo ili ambalo ni kama Ugonjwa kwenye jamii Zetu pamoja na kulikemea kuwa si jambo zuri kwa Vijana pamoja na Watu Wete kwasababu ni Uharibifu wa Maadili.

Msanii amepiga Vita Suala la Rushwa. Pia msanii ameweza kuonekana ni tabibu wa Magonjwa Sugu kwa kupiga Vita rushwa kupitia diwani hii imeonekana katika Shairi la "Rushwa" Mwandishi amezungumzia kuwa ni Vizuri kupokea na kutoa rushwa kwenye jamii kwasababu huchangia kupokea kwa halsi na Usawa wa Watu.

Msanii amezungumzia umuhimu wa kulipa deni. Pia katika kazi hii ye fasihi Mwandishi ameweza kuzungumzia umuhimu wa kulipa deni kupitia Shairi la "Dawa ye deni kulipa" Mwandishi anetumia njia hii kuwazungumzia na kuwaonya Wale Watu ambao Wanapokopa pesa Wanakuwa Wanyenyekevu ila Wakati wa kulipa deni huwa Wasumbufu.

Umuhimu wa Malezi bora. Msani ameweza kuonesha umuhimu wa Malezi bora na hii hufanye kumuonyesha Msanii kama tabibu wa Magonjwa Sugu kupitia Shairi la "Vijana wa Zanzibar" Mwandishi ameweza kuonesha umuhimu wa kuwaheshimu Wazazi pamoja na Malezi ~~yey~~ yaliyo bora kutoka kwa Mzazi au Mlezi kwenda kwa Mtoto ~~amp~~ ambapo hufanye jama iwe bora. Kwa kumalizia na diwani ya "Chungu tamu" jinsi Msanii wa Ushairi ni tabibu wa Magonjwa Sugu.



3. Msanii kupinga Vita kuala la Matabaka.
Pia kupitia duwani hii Muwandishi we kazi ya fasihi ameweza kuonesha Matabaka yeliyopo katika jamii kupitia shairi la "Chatu na kuku" hii ni hali ya kuwepo kwa Matabaka Mitangani mwa Watu katika jamii inaweza kuwa tabaka tawala na tawalwa katika Mfuko ya kila Sikia ya jamii zima.
Kuala la Uongozi. Muwandishi wa fasihi huweza kuonesha Matabaka yeliyopo kwenye jamii pia katika upande huu Msanii ameonekana kama tabibu wa Magonjwa sugu hii ni kutokana na kuonesha ya Matabaka yafaayo kwenye jamii pamoja na njia za kuyatatua Matabaka hayo kwenye jamii Zetu.
Msanii kuzungumzia kuala la kupitia Muhanga. Pia hii nayo huweza kuonekana kwa Watu ambao huweza kupitia Muhanga kwenye jamii Zetu kwa mfano Mafa ama nyingine ambayo hufanya Watu kwa na Ujasiri kupitia shairi la "Dakitari askari" pia kupitia shairi hii inaweza kuonesha jinsi Umuhimu wa kupitia Muhanga ambayo unafaa katika jamii.
Msanii kupinga Vita ukoloni mamboleo.
Pia Msanii anaweza kuwa tabibu wa Magonjwa sugu kwetebatu huweza kupinga Mambo au Vitu ambayo si sahihi kwenye jamii Zetu pamoja na kwetu Mambo ambayo si sahihi kwenye jamii zetu za leta siku.
Pia katika upande au kuala zima la msanii kupinga Maovu yaliyoko kwenye jamii Zetu yapo mambo Mengi ambayo Msanii au Muwandishi kupinga au kusiritiza sisi ya Umuhimu wa kitu kilam kwenye jamii.

Kielelezo 3.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kutoa baadhi ya hoja ambazo maelezo yake yanapingana na kauli kuwa, "Msanii wa ushairi ni tabibu wa magonjwa sugu yaliyopo kwenye jamii".

Aidha, watahiniwa wachache sana, sawa na asilimia 0.6 walipata alama za chini kuanzia 0 hadi 6 kutokana na kutoa hoja zisizo sahihi katika kuthibitisha kauli " Msanii wa ushairi ni tabibu wa magonjwa sugu yaliyopo kwenye jamii" kutokana na kutoelewa ujumbe

uliowasilishwa na wasanii katika diwani husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kutoa utangulizi na pia katika kiini cha swali alijadili dhamira mbalimbali badala ya kuthibitisha kauli aliyopewa. Vilevile, katika hoja zake hakuweza kutoa mifano ya mashairi ili kushadidia hoja alizotoa. Pia alishindwa kutoa hitimisho linaloendana na kauli aliyopewa ambalo lingekuwa kama suluhisho la magonjwa sugu yaliyopo kwenye jamii kupitia diwani husika. Kielelezo 3.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali.

Kielelezo 3.3



3 Kuthibitisha kuwa ushairi ni tabibu
wa magonjwa sugu yaliyopo kwenye
jamii.
Kwa kutumi vitabu viwili nili
vyosoma na thibitisha kama ifuatavyo
Nikianza na ~~dw~~ ushairi wa-
"chungu tamu" ushairi huu umeo-
nyesha namna ya kuondokana na
Uongozi mbaya; Theobald
A. Mvungi anaelezea namna ya-
kuukimbia na kupigana na uongo
zi mbaya uliopo madarakani.
Hivyo ndio maana tunasema ushai
ri ni tabibu wa magonjwa ya uovu.
Tabia mbaya ya wanaume-
kutembea na wake za watu;
Mwandishi anakemea katika ushairi
huu kuacha tabia ya kuiba wana
wake za watu wasije pata madhara.
Ndio maana tunasema ushairi ni -
tabibu wa magonjwa sugu
Maringo kwa akinadada
wanaputafutwa na wanaumewa kuwaoa
Mwandishi anaikemea tabia hiyo-
kwa kupitia ushairi huu kuwa wada
da wasiringi kwani wanaweza kuba
Ki~~ki~~ biza kuolewa. Hivyo ndio-
maana nakubali usemi wa msanii.



3. Nikifuatia na hoja za kutoka katika ushairi wa "fungate tamu" msanii ameeleza yafuatayo:

Ukoloni mambo leo; msanii ameweza kuwaonesha wanajamii kuwa pamoja na kwamba tumepata uhuru lla bado viongozi waliopo madarakani wanaendeleza tabia za ukoloni. Hivyo jamii inajua kuwa llishapata uhuru lakini bado inata waliwa.

Utawala wa kimabavu; msanii ameionesha jamii kwa kupitia ushairi kuwa kuna viongozi wanaopenda kutawala kimabavu. wakishachaguliwa hawapendi kusikiliza ushauri wowote ule hata kama wanakosea.

Ufujaji wa mali za umma pia msanii ameonyesha viongozi wanavyotumia pesa ya serikali ovyo bila kujali wananchi wao. umaskini upo pale pale. na huwa daugamyia utajili wa majengo yana yoonekana kuwa nchi ni tajiri.

Hivyo ndivyo msanii aliyo onyesha utabibu wa ushairi wa katika magonjwa ambayo ni maovu yanayotendeka serikalini.

Kielelezo 3.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuthibitisha kauli isemayo, “Msanii wa ushairi ni tabibu wa magonjwa sugu yaliyopo kwenye jamii na kupata alama za chini.

3.3.2 Swali la 4: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* na lilihusu uhakiki wa vitabu teule vya ushairi. Swali hili lililenga kupima uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha usemi usemao; " Washairi hutumia taswira kama zana ya kufikisha ujumbe kwa jamii waliyokusudia" kwa kutoa mifano minne ya taswira kwa kila kitabu katika diwani mbili alizosoma na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wachache (42.3%) kati ya wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa la kuchagua. Asilimia 98.4 ya watahiniwa hao walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani na kulifanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.



Chati Na. 9: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Kati ya watahiniwa waliojibu vizuri swali hili, asilimia 85.0 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 19 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu taswira mbalimbali zilizopo katika diwani teule. Miongoni mwao, asilimia 16.4 walijibu vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 17 hadi 20. Watahiniwa hao waliweza kubaini taswira na kuzielezea kwa mifano jinsi washairi walivyozitumia kufikisha ujumbe kwa jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja kwa kutumia diwani ya "Kimbunga" alitoa taswira kama vile; *Dumizi, Punda, Kimbwangai* na *Kimbunga*; na katika diwani ya "Chungu Tamu" alitoa taswira kama vile; *Chungu, Chatu, Tamu* na *Kuku*; huku akizitolea ufafanuzi mzuri wa namna zilivyofikisha ujumbe kwa jamii na kutaja mifano ya mashairi yaliyotumia taswira hizo kwa usahihi. Kielelezo 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vizuri na kupata alama za juu.

Kielelezo 4.1

4 kuishiria watu wasio na shukurani hata ukiwafanyia mema. Kwa kupitia taswira hii mwandishi anatoa ujumbe kuwa kuna watu kwenye jamii zetu hawana shukurani hata ukiwafanyia mema wanaweza kukutangazia vibaya.

~~Kibw~~ Taswira Ya Kibwangai; Taswira hii ipo katika shairi la KIBWANGAI ambaye inaonesha kuwa ni nyani ambae alipewa mgum na kuwa binadamu ili awatete nyani wenzie, lakini baada ya kufika kwenye jamii ya watu akajisahau, na kuacha kupigania haki za nyani wenzie. Huyo hii ni taswira inayoonesha Viongozi ambao wamechaguliwa lakini wakishapata madaraka wanawasahau wananchi waliowaweka madarakani. Huyo kwa kutumia taswira hii Mwandishi anatoa Ujumbe kuwa kuna baadhi ya Viongozi wanasahau majukumu yao wakiingia madarakani.

Taswira Ya Kimbunga; Kimbunga ni upepo mkali ambao ukitokea unaweza kubadili hali ya hewa na kuleta mabadiliko, Taswira ya kimbunga kama ilivyotumika katika shairi la KIMBUNGA inaonesha ~~Mabadiliko~~ Mapinduzi yaliyofanyika Zanzibar ambayo yalikuwa na dhumuni la kuleta Usawa miongoni mwa wananchi. Huyo kwa kutumia taswira hii mwandishi anatoa Ujumbe ili kuleta mabadiliko katika jamii ni lazima watu

4. wafanye mapinduzi

Vilevile kwenye riwaya ya CHUNGU TAMU, mwandishi ametumia taswira ili kutoa Ujumbe kama ifuatavyo

CHU Taswira ya CHUNGU; Chungu ni taswira iliyopo kwenye shairi la Chungu tamu. Kiuhalisia kitu kichungu ni kitu kibaya chenye ladha mbaya. Kwenye kitabu imetumika kuonesha machungu ka Vile Kushwa, Usaliti. Huyo kwa kutumia taswira hiyo mwandishi anatoa Ujumbe pia kuwa kuna mambo mabaya ambayo yapo katika jamii na inabidi yapigwe Vita

Taswira ya CHATU; Hii ipo kwenye shairi la CHATU NA KUKU, hii ni taswira inayoonesha wanyonyaji katika shairi hili tunaona jinsi chatu alivyokuwa akila kuku mmoja badala ya moingine, Hii inaonesha unyonyaji. Mwandishi kwa kutumia taswira hii anatoa Ujumbo kwa watu wa tabaka la juu wanawanyonya sana watu wa tabaka la chini

Taswira ya TAMU, taswira hii ni kwenye shairi la CHUNGU TAMU, ambapo kiuhalisia kitu kitamu ni kitu chenye ladha nzuri na kizuri, Tamu ni taswira iliyotumika kuonesha mambo mazuri yaliyopo kwenye jamii kama Vile Mapenzi, Ndoa, Mapinduzi. Huyo mwandishi anatoa ujumbe kuwa japokuwa kuna mambo mabaya ila hata mazuri yapo.

4. Taswira ya kuku; Ni taswira iliyotumika kuonesha wanyonywaji yaani tabaka la chini wanaonyonywa na tabaka la juu. Kwa kupitia taswira hii Mwandishi anatoa ujumbe kuwa watu wa tabaka la chini hawakohum kufanya mambo ya kujiletea maendeleo.

Huyo Taswira katika kazi ya fasihi na mchango mkubwa kwa kutoa taarifa au Ujumbe juu ya fwala fulani hualotendeka kwa jamii husika.

Kielelezo 4.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeelezea taswira mahsusi katika diwani ya “Kimbunga” na “Chungu Tamu” na kutoa mifano ya jinsi zilivyotumika kama zana ya kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa.

Watahiniwa wengine katika kundi hili asilimia 13.8 walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kwa kuwa waliweza kutoa baadhi tu ya hoja kwa usahihi na nyingine hazikujitosheleza kwa mifano au nyingine maelezo yalikuwa hafifu na hivyo kutokidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa taswira kutoka katika diwani ya "Chungu Tamu" kama vile; *Chatu, Punda* na *Ngamia* ambazo zilikuwa sahihi lakini akatoa taswira nyingine kama 'Nuglu na watwana" ambazo hazikuwa sahihi kulingana na matakwa ya swali. Hata hivyo, katika diwani ya “Fungate ya Uhuru” alitoa taswira sahihi kama vile; *Fungate, Kunguru, Mjamzito* na *Viongozi wa Afrika*; japokuwa alitoa maelezo yasiyojisheleza kuhusu taswira hizo na kupata alama za wastani. Kielelezo 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 4.2



4 Taswira - Ni ujumbe unaowakili
shwa au kuwasilishwa kwa kutumia
picha mbalimbali.
Kwa kuanza na mashairi ya CHUNGU
TAMU iliyoandikwa na THEOBALD
A. MVUNGI tunaweza kuona taswi
ra mbalimbali. Kama vile.
Chatu, Mwandishi theobald
mvungi ametumia taswira ya
chatu kuelezea jinsi wakoloni
waliwyo kuwa wanatunyonya na
wanavyo tunyonya kupitia taswira
ya chatu tunaweza kuona kuwa
ukoloni au wakoni ni watu
wanaoperekea kikwazo cha maendeo

4 Nuglu- Mwandishi anatueleza kuwa nuglu ni sehemu ya kijiji ambacho bado hakijaendelea. hivyo mwandishi ameweza kutumia nuglu kwa kuweza kuonyesha kuwa umaskini bado upo na upo hasa sehemu za vijijini hivyo basi hatuna budi kupambana ili kuondokana nao.

Punda na ngamia, Mwandishi ametumia picha ya ngamia na punda kwa kueleza namna watu wanavyoonewa, wanavyonyanyashwa na kiongozi au watu watabakala juu hivyo kupitia punda na ngamia tunaona jinsi uonevu bado upo.

Watwana, Xi watu ambao wa na taka mabadiliko hivyo tunaweza kuona kuwa Mwandishi analenga ujumbe kuwa wanataka mabadiliko katika jamii

Kwa kutumia ~~tam~~ ~~kwa~~ Mashaino ya JUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na MOHAMED S. KHATIBU tunaweza kuona ~~dhamira~~ ~~twasira~~ mbalimbali

Jungate- xi ulimbeende wa Mahanisi ambao unavekwa ndani siku saba. pia Jungate ni kama sikukuu kula na kusaza Mwandishi ameweza kutumia Jungate kwani anaelezea jinsi kiongozi wanavyo ongoza yibaya katika shairi la Jungate tunapa: uongo-



4 zi mbaya hivyo shairi la Jungate
linataka viongo wawe wanaongoza
vizuri.
Kunguru- Mwandishi ametumia
twaswira ya kunguru kwa kutoonye
sha tabia za ukoloni mambolea
bado upo na unaendelea katika nchi
yetu hiyo basi ukoloni mambolea
ni kikwazo cha maendeleo katika
taifa.
Mjamzito- Mwandishi theobaldy
ametumia taswira ya mjamzito ili
kuonyesha jinsi anibavyo bado kuna
viongozi ambao ni waoga katika
jamii yetu. Hivyo tunapata ujumbe
kama kiongozi hapaswi kuwa mwoga
Viongozi wa Afrika, pia Mwandishi
ameweza kutumia taswira ya ~~wa~~ viongo
wa Afrika ilikweza kuonyesha uovu
uliopo kwa hawa viongozi. Hivyo
katika taswira ya ~~wambo~~ ~~wetko~~
viongozi wa Afrika tunapata ujumbe
kwamba viongozi wanapaswa kutenda
yaliyo mema.
Kwa ujumla tunaweza kuona
kwamba taswira zimewekwa kwa
lengo la kufikisha ujumbe katika
jamii hivyo taswira haziepukiki
kwani hupunguza ukali wa maneno

Kielelezo 4.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetaja na kuelezea baadhi ya taswira jinsi zilivyotumika kama zana za washairi kufikishia ujumbe kwa jamii kwa usahihi na kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache sana (1.2%) kati ya wote waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6 kutokana na kushindwa kubaini kwa usahihi taswira na kuonesha jinsi zilivyotumika kama zana za kufikishia ujumbe kwa jamii kupitia diwani teule walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijadili dhamira mbalimbali katika diwani ya “Kimbunga” kinyume na matakwa ya swali. Mtahiniwa huyo alitoa taswira kama vile; *uongozi mbaya, kuwepo kwa kuingiliana katika ndoa, tatizo la kutokuwa na shukrani na kuwepo kwa umuhimu wa kusheherekeana*; na katika

diwani ya “Fungate ya Uhuru” alitoa taswira kama vile; " *Taswira juu ya tatizo la kuingilia ndoa za watu, kuwepo mapenzi ya thati, kuwepo kwa dharau na kuwepo kwa uongozi mbaya*" ambazo zilikuwa kinyume kabisa na matakwa ya swali. Kielelezo 4.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha taswira mbalimbali zilizotumiwa na washairi wa diwani ya “Fungate ya Uhuru” na “Kimbunga.”

Kielelezo 4.3



4 Taswira ni ile ishara inayopatikana baada ya kusoma kazi ya fasihi. Pia inaweza kutokea baada ya kusoma beti fulani ya mtu au matukio mbalimbali ~~ya~~ anayoyafanya. Wasemi huu umethibitishwa kupitia vitabu viwili kati ya "KIMBUNGA" muandishi Haji Gora na diwani ya "FUNGATIA YA UHURU" muandishi Mohamed S. Khatibu. Kwa kuanza na diwani ya "KIMBUNGA" muandishi ameweza kuonesha taswira mbalimbali ili kufikisha ujumbe kwa jamii kama tufatavyo.

Taswira juu ya kuwepo uongozi mbaya. Kupitia taswira muandishi ameweza kuonesha kuwa ni dhana ya kufikisha ujumbe kwa jamii, ~~ujumbe~~ Hii imethibitika kupitia shairi la "KUJIITAWA" tuneuona wazi kuwa kuna viongozi ambao huongoza raiya wao vibaya. Ujumbe ~~wa~~ ni kuwa uongozi mbaya unapaswa

4 kutumia taswira hii kama nyenzo ya kufikisha ujumbe kwa jamii. Hii imethibitika kupitia shairi la "PAKA SHUME" ambapo tunaona wazi kuwa kuna baadhi ya watu huingitia ndoa za watu, kupitia taswira tunapata ujumbe kuwa sivizuri kuingitia katika ndoa za watu.

Taswira juu ya kuwepo mapenzi ya thati. Mshairi wa diwani hii ya fungatia ya uhuru ametumia taswira hii kama ni nyenzo ya kufikisha ujumbe kwa jamii. Hii imethibitika kupitia shairi la "WEWE PEKE YAKO" ambapo tunaona wazi kuwa kuna baadhi ya watu huwa na mapenzi ya thati kwa wanawake wao, kupitia taswira hii tunapata ujumbe kuwa, mapenzi ya thati ni muhimu katika ndoa.

Taswira juu ya kuwepo dharau. Mshairi ameweza kuitumia taswira hii kuwa ni nyenzo ya kufikisha ujumbe kwa jamii. Hii imethibitika kupitia shairi la "BIMBI" ambapo kuna baadhi ya watu huonekana kuwa na dharau. kutokana na hali zao walizonazo, kupitia taswira hii tunapata ujumbe kuwa dharau ni majanga ya ugomvi katika jamii.

Taswira juu ya kuwepo kwa uongozi mbaya katika jamii. Mshairi wa diwani hii ameweza kuitumia taswira hii kama nyezo ya kufikisha ujumbe katika jamii. Hii imethibitika kupitia shairi "KUJITAWALA" ambapo kuna baadhi ya viongozi huongoza vibaya uongozi wao halimae kupelekea migogoro katika jamii. kupitia taswira hii mshairi ameonesha ujumbe kuwa uongozi mbaya ni chanzo cha kurudisha

4 nyuma maendeleo ya jamii kiujumla.

Kwakufungia, kutoka na hali yote ambayo mshairi ~~wamewe~~ wametumia taswira mbalimbali kama nyenzo ya kufikisha ujumbe kwa jamii, hivyo basi tunapaswa kufuata yale yote ambayo yanafaa kufatwa katika jamii na kuachana na yale yote ambayo hayafai katika jamii.

Kielelezo 4.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejadili dhamira badala ya taswira kulingana na matakwa ya swali na kupata alama 0.

3.4 SEHEMU C: RIWAYA

3.4.1 Swali la 5: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* na lilihusu uhakiki wa vitabu teule vya riwaya. Swali hili lililenga kupima tathmini na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kauli isemayo "Hakuna kiumbe asiye na ila" kwa kutoa hoja mbili za uzuri na mbili za kasoro za mhusika mkuu kwa kila kitabu kati ya riwaya mbili alizosoma na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Zaidi ya nusu ya watahiniwa (72.9%) waliofanya mtihani walichagua swali hili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri sana ambapo asilimia 99.5 walipata alama nzuri na za wastani yaani kuanzia 7 hadi 19 na kulifanya swali hili kuwa na kiwango cha juu zaidi cha kufaulu kuliko maswali yote yaliyotahiniwa katika mtihani huu. Chati Na. 10 inaonesha bayana viwango vya watahiniwa vya kufaulu kwa asilimia.



Chati Na. 10: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 94.8 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 12 hadi 19 kwa kuwa waliweza kutoa hoja zinazoelezea uzuri na kasoro za mhusika mkuu ili kuthibitisha kauli inayosema; "Hakuna kiumbe asiye na ila" katika riwaya mbili teule. Miongoni mwao, asilimia 27.5 walijibu vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 17 hadi 19. Kiwango hiki kizuri cha kufaulu kinadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa mahsusi kuhusu wahusika wa riwaya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja katika riwaya ya “Mfadhili” kwa kuelezea uzuri wa mhusika mkuu Dania

kama vile; *mchapakazi na mwenye mapenzi ya dhati* na hoja mbili za kasoro za mhusika huyu kama vile; *mtu mwenye chuki na asiye na msimamo* hoja ambazo ni sahihi kulingana na wasifu wa mhusika huyo. Pia katika riwaya ya “Vuta N'kuvute” alielezea uzuri wa mhusika mkuu "Yasmini" kama vile; *mtu mwenye mapenzi ya dhati na jasiri"* na kubainisha kasoro mbili za mhusika huyo kama vile*; mvivu na msaliti* hoja ambazo zilikidhi matakwa ya swali ipasavyo. Kielelezo 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kutokana na kukidhi matakwa ya swali.

Kielelezo 5.1



5.4. "Hakuna kiumbe asiye na ila" usemi huu ni kweli kwani kila kiumbe ana uzuri na ubaya wake. Kwa kutumia riwaya mbili yaani MFADHILI pamoja na VUTA N'KUVUTE kila msanii ameweza kuonesha uzuri pamoja na udhaifu wa mhusika mkuu. Kwa kuanza na mhusika mkuu katika kitabu cha MFADHILI yaani Dania amebainika kuwa na uzuri pamoja na udhaifu kama ifuatavyo:

Dania alikuwa ni mchapakazi. Mwandishi amemwonesha mhusika huyu akiwa na bidii katika kazi kabla ya kupatwa na matatizo mbali mbali kama vile kusalitiwa na Jerry, lakini pia Dania alikuwa mchapakazi kabla ya kuwa mlevi na kabla ya kuugua.

Dania alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Jerry. Pia msanii amemwonesha Dania kama mhusika mkuu akiwa na mapenzi ya dhati kwa Jerry, naliyo maana akaamua kurudiana naye mara baada ya kurudi kutoka marekani na alikuwa anampenda sana

54. Kama ~~mto~~ baba wa mwanaye junior.
Hivyo msanii amemwoneshe Dania
kama mhusika mkuu akiwa na mapen-
zi ya dhati. Licha ya kuwe na
uzuri Dania pia alikuwa na
kasoro zifuatazo:
Dania alikuwa na chuki.
Msanii amemwonesha Dania kwa-
kuonesha kuwe mara baada ya
Dania kuugua, ofisi yake ilichukutiwa
na Gaddi, na mara baada ya Dania
kupona ilibidi aruali kazini kwake
na kumkute Gaadali Bullah mara
baada ya Dania kuulize jina Gaddi
alijibu "Naitwa Gaddi Bullah"
Dania alidiriki kumwambia Gaddi kuwa
"Wewe ni Gaiddi Bullah" lakini
pia kiteralo cha Dania kumfukuza
Gaddi mezani ni sehemu ya chuki
ambayo ilikuwa nalani ya Dania.
Dania alikuwa hana msimamo.
Mhusika huyu ameoneshwa na msanii
akiwe hana msimamo kaufike, suala
la mapenzi, kwani, kwa mara ya
kwanza, aliteralwa na Jerry, lakini
mara baada ya Jerry kuruali
kufoka marekani Dania alirubuniwa
na kukubali kurudiana na Jerry
na kumfosa Gaddi Bullah. Hivyo
mhusika huyu ameonekana kuko
sa msimamo kaufika suala la
mapenzi. Licha ya Dania kutu-



Kielelezo 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuthibitisha kauli “Hakuna kiumbe asiye na hila” kwa kutoa hoja sahihi kuhusu uzuri na kasoro za wahusika wakuu wa riwaya mbili teule**.**

Watahiniwa wachache, asilimia 4.7 walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza ama kwa kutaja baadhi ya wahusika ambao si wakuu au kuwaelezea wasifu usiostahili na bila kutumia mifano halisi kutoka katika riwaya husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia riwaya ya

“Mfadhili” na kutoa kasoro mbili za mhusika mkuu Gadi Bullah kuwa; *alikuwa mlevi wa sigara na pombe*, hoja ambazo si sahihi kulingana na wasifu wa mhusika huyo. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kutoa wasifu wa baadhi ya wahusika usio sahihi kulingana na uhusika wao katika riwaya husika.

Kielelezo 5.2



5 Mhusika mkuu; Ni aina ya mhusika
ambae yeye anakua akiongelewa kuanzia mwanzo
wa hadithi mpaka mwisho. Ni kweli kwamba
"Hakuna kiumbe asiye na ila". Kwa kutumia
riwaya ya MFADHILI" iliyo andikwa na Hussein
Tuwa pamoja na YUTA N'KUUUTE iliyo andikwa na
Shaji Adam Shaji. Na kwakumtumia mhusika
mkuu ambea ni Ghadi Bullah kutoka katika riwaya
ya MFADHILI, pamoja na DENGE kutoka katika
riwaya ya YUTA N'KUUUTE, Wanathibitisha kauli hii.
Kwa kuanza na uzuri wa Ghadi Bullah kutoka
riwaya ya MFADHILI
Mchapakazi; katika riwaya ya
MFADHILI, Ghadi Bullah alikua ni muhusika
mkuu ambae alikua mfanyakazi mzuri katika
kampuni ambalo lilikua ni lakukusanya kodi
Ghadi Bullah alikua ni meneja ambae alikua
ni mchapakazi ambae anafaa kuigwa na jamii.
Hivyo basi jamii haina budi kuiga uzuri wa Ghadi
Bullah katika ufanyaji kazi kwani utaleta maendeleo.
Mapenzi ya dhati; Ghadi Bullah katika
riwaya ya MFADHILI alikuwa ni muhusika mkuu
ambae alikua anamapenzi ya dhati kwa mke
wake Nyambuje ambae alikuja kumsaliti, Nakua na
mapenzi ya dhati kwa Daania ambae nae Daania ali
kuja kumsaliti Ghadi Bullah. Hivyo basi uzuri
wa Ghadi Bullah wa kuwa na mapenzi ya dhati
watu katika jamii wanatakiwa kuuiga kwani
unafaa katika jamii.
Pia Ghadi Bullah alikua na kasoro zake

5 Ulevi; Hii ilikua kasoro ya Ghadi Bullah kwani alikua ni mlevi wa sigara na pombe ambazo zilimpelekea mpaka akasimami shwa kazi na baadae kuhamishwa kituo kutokana na kutia hasara kampuni kwa sababu ya ulevi. Hivyo basi hii ni kasoro ya Ghadi Bullah.

Kuchanganya mapenzi na kazi; Hii pia ni kasoro ya Ghadi Bullah kwani yeye alikua akichanganya masuala ya kimapenzi na kazi na baadae kupelekea kampuni kupata hasara. Hivyo hii ilikua ni kasoro Ghadi Bullah ambayo alikua anayo na ilikua kasoro mbayo.

Na mhusika mkuu katika riwaya ya YUTA N'KUVUTE ambeye ni DENGE alikua na uzuri wake na kasoro zake. Na zifuatazo ni uzuri wa Denge.

Kupinga ukoloni; Denge alikua ni mhusika mkuu ambae alikua anapinga suala la ukoloni ambalo lilikua likiendeled ~~de~~. Denge alikua akipambana na wakoloni bila ya kujali wala kuhofia choche. Hivyo huu ni moja kati ya uzuri wa Denge.

Ujasiri; Huu pia ni uzuri wa ~~deng~~ Denge kwani denge alikua ni jasiri ambae alikua hao gopi wakoloni wala askari walikua wakimtafuta inspetta wright na muwenzake walikua wakimtafuta Denge na Denge alikua hawaggopi kuta kidogo. Hivyo pia huu ni uzuri ambao ~~ya~~ unaya kuigwa na jamii.



5 Pia Denge alikua na Kasoro zake
Kwani "Hakuna Kiumbe asiye na ila". Na yaguatayo ni Kasoro za Denge.
Hakua na mapenzi ya dhati; Hii ni moja
ya Kasoro za denge Kwani yeye alikua
Hana Mapenzi ya dhati Kwa ~~Yasmini~~ Yasmini
yeye alikua akifanya Kazizake za Kupambana na
wakoloni hakujali Ku husu penzi ~~ke~~ lake
Kwa Yasmini. Hivyo hii ni Kasoro ya denge
ambayo haifai Kuigwa.
Mlevi; Pia hii ni Kasoro ya Denge
Kwani alikua ni mlevi yeye pamoja na
marafiki zake walikua wanapenda starehe.
Hivyo hii Kasoro ya denge ya ulevi hai-
fai Kuigwa Katika jamii Kwani sio tabia
nzuri mtu kua mlevi.
Hitimisho; "Hakuna Kiumbe asiye na
ila" kauli hii ni ya Kweli Kwani pia Katika
jamii ambazo tunaishi watu wote huwa na
mazuri ambayo wanakua nayo na pia huwa
na mabaya ambayo ankasoro ambazo wa
hakua nazo.

Kielelezo 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa yenye mapungufu katika hoja zake na makosa ya kitahajia kwa kuandika *Ghadi* badala ya Gadi na *denge* badala ya Denge kutokana na kutozingatia taratibu za uandishi ipasavyo.

3.4.2 Swali la 6: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* na lilihusu uhakiki wa vitabu teule vya riwaya. Swali hili lililenga kupima tathmini na lilimtaka mtahiniwa kufafanua usemi usemao, “Taifa litajengwa na watu wenye moyo” kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu kwa kutumia riwaya mbili alizosoma, na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wachache yaani asilimia 29.9 kati ya wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali la

kuchagua. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana ambapo asilimia 99.2 walikuwa na kiwango kizuri na cha wastani cha kufaulu. Chati Na. 11 inaonesha viwango vya watahiniwa vya kufaulu kwa asilimia.



Chati Na. 11: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Kiwango kizuri cha kufaulu kwa watahiniwa kinaonesha kuwa asilimia 93.2 walijibu vizuri swali hili kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu katika kufafanua usemi usemao, "Taifa litajengwa na watu wenye moyo" na kupata alama kuanzia 12 hadi 19.5. Kiwango hiki kizuri kinaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu *wahusika chanya* katika riwaya teule na jinsi walivyotumiwa na waandishi katika harakati za kujenga taifa bora. Miongoni mwao, asilimia 28.7 walijadili kwa ufasaha harakati za wahusika walioonesha kuwa na moyo wa ujenzi wa taifa lisilo na *ubaguzi, uonevu, uvivu, matabaka na uongozi mbaya* na hivyo kupata alama za juu kuanzia 17 hadi 19.5. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia riwaya ya "Vuta N'kuvute" na kufafanua jinsi wahusika walivyoonesha; *umoja na mshikamano, kujitoa mhanga, uwezo wa kufanya mapinduzi na mapenzi ya dhati.* Pia katika riwaya ya "Mfadhili" alionesha jinsi wahusika wanavyozingatia; *uongozi bora, uwajibikaji/bidii katika kazi, kupiga vita chuki na fitina na mapenzi ya dhati* kama nyenzo za kujenga taifa bora. Kielelezo 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

Kielelezo 6.1



6. "Taifa litajengwa na watu wenye moyo" usemi
huu unamaana kwamba ili kujenga taifa bora
lenye maendeleo kunahitajika watu watakao
kuwa tayari kufanya kazi hiyo bila kusali
jambo lolote. katika riwaya ya "Mtadhili" iliyo-
andikwa na Hussein Tuwa na Vuta N'kuvute"
iliyoandikwa na shafi Adam shafi waandishi
hawa wameweza kueleza ni kwa namna
gani watu katika jamii wanavyowaza kufanya
mambo mbalimbali ili kujenga jamii
kwa kuanza na riwaya ya "Vuta N'kuvute"
mwandishi ameeleza namna watu wenye moyo
wanavyosaidia kujenga taifa.
Umoja na ushirikiano. katika kujenga
taifa ni dhahiri kuwa umoja na ushirikiano
unatakiwa kama ambavyo imeonekana kwa
Denge, mambo, sukutua na maratiki cao
wengine katika kuhakikisha wanafanikisha
kusambaza taarifa mbalimbali kuhusiana
na serikali ya kikoloni kisiwani kwao
Hivyo basi watu wenye moyo ni lazima
washirikiane ili kujenga taifa.
Kujitoa Muhanga. katika riwaya
hii mwandishi anaeleza namna Denge alivyo
jitoa muhanga kufa kupona katika
kupambana na wakoloni hakuogopa kitu
chochote ndio maana hata akikamatwa
na kutishiwa vikali na maaskari alikuwa
hajali chochote, yeye alitaka kuhakikisha
ukoloni unatoweka nchini mwao. Huta
katika jamii zetu watu ni lazima wawe
tayari kusitoka kwa maendeleo ya taifa

6 Umuhimu wa kufanya mapinduzi.
katika riwaya hii mwandishi anaeleza
kuwa watu wenye moyo ndio watakosenga
taifa kwani watakuwa tayari kufanya
mapinduzi kwa mfano Yasmini alikuwa
ni mwanamapinduzi kwani aliweza kutetea
mila zile zilizomkandamiza mwanamke
kama vile kuchagulwa mume pia Denge
alifanya mapinduzi suu ya serikali ya kikoloni
Mapenzi ya dhati. Mwandishi anaeleza
kuwa watu wenye moyo katika ujenzi wa taifa
ni lazima wawe na mapenzi ya dhati kwa
Mfano mapenzi ya dhati ya Bukheti kwa
yasmini pia mapenzi ya dhati ya Yasmini
kwa Denge lizha ya kuwa Denge ha kuwa
na pesa lakini alihakikisha anaendelea
kumpenda
pia katika riwaya ya "Mtadhili"
Mwandishi anathibitisha usemi huu kama
ufuatavyo
Umuhimu wa Uongozi bora. Mwandishi
anaeleza kuwa mtu mwenye moyo na taifa
lake ni lazima ajue umuhimu wa uongozi
bora ili kuleta maendeleo Mfano Mama
Mlole alikuwa kiongozi bora sambo lililo
mfanya aweze kuwathamini wafanyakazi
wake na kuwapenda. Hata katika jamii
zetu wapo watu wenye moyo wa dhati
na taifa letu hivyo huweza kufanya
uongozi wao kwa manufaa ya watu
wote wala siyo pekee yake kwa
maendeleo ya taifa.



6. Uwasibikasi na bidii katika kazi. katika
riwaya hii mwandishi anaeleza namna watu
wenye moyo, na taifa wanavyo wasibika katika
nafasi zao kwa mfano Gaddi na Dania
walifanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa
sambo lilifanya kusamehewa ata pindi
walipokosea. Hata katika jamii zetu ni
lazima kazi zifanywe kwa bidii zli kusenge
jamii zetu.
Kupiga vita chukina Ritina. katika
riwaya hii mwandishi anaeleza namna
chuki znavyo kwa misha maendeleo ya taifa
kwa mfano B. Hanuna alikuwa na
Chuki kwa Dania na Nunu lakini
Chuki hiyo zlimalizika na maisha yakaen
deleo. Hata katika jamii zetu chuki
na Ritina ni lazima ziwekwe kando kwa
maendeleo ya taifa
Mapenzi ya dhati. Mwandishi
anaonesha kuwa katika ujenzi wa taifa
watu ni lazima wawe na mapenzi ya
dhati kama zlivyositokeza kwa Gaddi.
Gaddi alimpenda sana Dania licha ya
kwamba alimwaliti lakini alizimua kutoa
lni lake zli kuokoa maisha yake. Hata
katika jamii zetu watu ni lazima tuwe
na mapenzi ya dhati zli tujenge taifa
"Taifa litajengwa na wenye moyo" kwani
wao hutambue thamani ya taifa lao lakini
wasio na moyo ni lazima wakakwa misha
maendeleo hayo kwa kusihwisha na
rusha, unvu hata mongozi mbaya.

Kielelezo 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja sahihi nne kwa kila kitabu katika riwaya ya “Vuta N'kuvute” na “Mfadhili” katika kufafanua usemi usemao, “Taifa litajengwa na watu wenye moyo.”

Aidha, watahiniwa wachache, (6.0%) walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa baadhi ya maelezo yasiyojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika riwaya ya

Vuta N'kuvute alitoa hoja kuhusu tabia za wahusika bila maelezo yenye kufafanua ni kwa jinsi gani taifa hujengwa na wahusika hao, hivyo kupata alama za wastani kama kielelezo 6.2 kinavyodhirisha.

Kielelezo 6.2



6 Taifa ni sehunu ambayo wanaishi watu am
bao wapo Chini ya utawala unao wawongoza. Ni
kweli kwamba Taifa lifeyengwa na watu wenye
moyo.
Kwa kutumia riwayaya MFADHILI zifuata
zo ni hoja zinazothibitisha usemi huu riwaya
hii imeandikwa na HUSSEIN TUWA
Mama mlole, huyu ni mhusika anaye onekana
kama ni mwongoni mwa watu watakao lyenga Tai
fa kwa kuwa alikuwa na moyo. Mama mlole ali
kuwa mwajibikaji katika kazi yake hata alipoene
kuwa kampuni yake inataka kumpoteza mtu
muhimu na muwajibikaji katika kazi alifanya
kilanjia ili awaze kumrudisha kazini ili awaze
kuendelea na kazi ya kulyenga Taifa. katika
jamii wakina mama mlole wapo
Gadibullah, alikuwa ni mtu ambaye mwe
nye moyo wa kulyenga taifa lake kwa kuwa
alikuwa ni mtu mwenye upendo, mvumilivu na
mchapakazi na siku zote taifa linayengwa na
watu wachapakazi, wenye upendo na wavumilivu
kama Gadibullah
Nunu, ni mwanamke mwenye uyasiri, mwe
nye upendo, mwajibikaji na pia ni mvumilivu huyu
alimsaidia sana rafiki yake Dania pindi ali
pokuwa kwenye matatizo na katika kulyenga
Taifa watu wenye moyo kama wa nunu wa
kuwasaidia watu wengine ndio wenye mchango
mkubwa katika kulyenga Taifa
Bi hanuna, huyu alikuwa ni dada yake
na Gadibullah alikuwa mtu anayesamehe, mtu
asiye na kinyongo katika kulyenga Taifa Bi



Kielelezo 6.2 kinaonesha majibu ya mtahaniwa aliyetoa ufafanuzi usiojitosheleza kimaudhui katika kuthibitisha usemi usemao "Taifa litajengwa na watu wenye moyo" na kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sana (0.8%) ndio waliokuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 6.5. kutokana na kutoelewa vyema matakwa ya swali hili. Watahiniwa hao walifafanua migogoro, falsafa, na matumizi mbambali ya lugha katika riwaya hizo bila kuzingatia wahusika na utendaji wao dhidi ya ujenzi wa taifa bora katika kuthibitisha usemi "Taifa litajengwa

na watu wenye moyo.” Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza migogoro katika aya ya kwanza na ya pili kutokana na kutoelewa kutoelewa matakwa ya swali. Pia, alitumia neno ushairi badala ya riwaya ya “Kufikirika,” na pia katika hoja nyingine alitumia tamthiliya ya “Nguzo Mama.” Kielelezo 6.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua migogoro na dhamira zisisizoeleweka kinyume na matakwa ya swali.

Kielelezo 6.3



SEHEMU C

6 "Taifa litajengwa na watu wenye moyo"
Usemi huu unadhihirika katika riwaya hizi mbili.
Kufikirika - Shaban Robert
~~Fut~~ Vuta N'kuvute - Shafi Adam Shafi

Falsafa hii inatiliwa nguvu sana katika riwaya hizi mbili.
Vuta N'kuvute - Riwaya hii ina watu wa wahusika katika kuonesha jinsi jamii inavyo pata migogoro wakati wa kulijenga Taifa: Migogoro kama vile Uporaji wa mali za umma, Rushwa na Ubadhirifu, Udanganyifu na Ulaji rushwa ni migogoro illyo tajwa katika riwaya ya Vuta N'kuvute: Katika ~~dhima~~ dhima hii ya kujenga Taifa wenye moyo wanata kiwa kupambana na maovu yote haya ili kulijenga taifa
Katika Ushairi wa Shabani Robert Kufikirika kuonesha madhira ya ~~ra~~ rushwa, matumizi mabaya ya fedha za bima mambo yanayofanywa na Viongozi wachache na kurudisha juhudi za kulijenga Taifa.
Tathmini ya Viongozi mbaya katika jamii limeelezwa katika riwaya zote mbili; Tunaona katika Kitabu cha "Nguzo mama" wanamama wanasambaratika na kugawanya biashara kufanya kila mmoja peke yake kutokana na


6 Uongozi mbaya.
Halikadhalika katika riwaya
ya Shaban Robert, Uongozi mbaya
umeelezwa kuwa nitatizo katika
jamii, hivyo jamii nilazima ipawe
elimu na kupata uongozi bora
ili kupata maendeleo

Kielelezo 6.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuthibitisha usemi “Taifa litajengwa na watu wenye moyo” kwa kujadili mambo yasiyohusu utendaji wa wahusika katika ujenzi wa taifa bora kupitia riwaya teule.

3.5 SEHEMU D: TAMTHILIYA

3.5.1 Swali la 7: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* na lilihusu uhakiki wa vitabu teule vya tamthiliya na lilimtaka mtahiniwa kueleza jinsi miisho ya tamthiliya isivyokidhi matarajio ya jamii kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu kwa kutumia tamthiliya mbili alizosoma. Swali lililenga kupima tathmini na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wachache sana ambapo asilimia 16.7 pekee ndio waliojibu swali hili la kuchagua. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa hao kilikuwa kizuri ambapo, asilimia 82.6 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na. 6 linaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kiasilimia.

Jedwali Na. 6 Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Watahiniwa	Asilimia ya Watahiniwa
0.0 - 6.5	592	17.4
7.0 - 11.5	1440	42.2
12.0 - 20.0	1375	40.4

Takwimu zilizowasilishwa katika jedwali zinaonesha kuwa, asilimia 40.4 za watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango

kizuri yaani kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 19. Kati yao, asilimia 7.3 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kutokana na kutoa majibu yaliyokidhi matakwa ya swali ipasavyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa utangulizi unaofafanua swali vizuri na katika kiini alieleza kwa usahihi jinsi miisho ya tamthiliya za "Morani" na "Nguzo Mama" isivyokidhi matarajio ya jamii. Katika tamthiliya ya "Morani" alitoa hoja kama vile; *kutokuwepo kwa suluhisho sahihi la viongozi wanaojishughulisha na rushwa, kutokuoneshwa kwa njia sahihi ya kuwaadhibu wahujumu uchumi wa nchi na kutoonekana kwa hatma ya mapambano ya morani dhidi ya uhujumu uchumi*. Kwa upande wa tamthiliya ya "Nguzo Mama" mtahiniwa huyo alitoa hoja kama vile; *kutooneshwa kwa njia sahihi zinazotakiwa kutumika ili kuinua nguzo mama, kutotolewa kwa suluhisho la unyanyasaji wa mwanamke na kutooneshwa hatma ya unyanyasaji wa wajane baada ya kufiwa na waume zao*. Mtahiniwa huyo pia alitoa hitimisho zuri linaloendana na swali husika. Kielelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

Kielelezo 7.1



7 Tamthiliya ni moja ya kazi za fasihi andishi ambayo huwa katika mtindo wa majibizano. Waandishi wengi humalizia tamthilia zao vibaya ambapo miisho hiyo inakuwa haikidhi matarajio ya jamii husika. Kwa kutumia tamthiliya ya MORANI iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo na tamthiliya ya NGUZO MAMA iliyoandikwa na Penina Muhando kuthibitisha ~~dai kati~~ jinsi miisho hiyo inavyokuwa haikidhi matarajio ya jamii.

Kwa kuanza na tamthiliya ya MORANI jinsi miisho isivyokidhi matarajio ya jamii.

7. Mwandishi hajatoa suluhisho sahii la Viongozi ambao Wanajishughulisha na Siasa la rushwa, Mwishoni mwa tamthiliya hii mwandishi ameonesha kuwa Viongozi ambao ni Mlemeta na Yusuphu Walidkuwa Wakijishughulisha na kupokea rushwa kutoka kwa Nungunungu Waliamishwa kituo cha kazi na kupelekwa nchi nyingine kusendelea na kazi, Hivyo basi suluhisho hili halikidhi Matarajio kwani Viongozi hao Hitakiwa Wahukumiwe kwa hiyo ya rushwa na siyo kuhamishwa.

Mwandishi hajaonesha njia sahihi ya kuwaa dhibu watu Wanajishughulisha na Ubugumu Uchumi wa nchi, kwani Mwandishi kwa mwisho wa kitabu ameonesha kuwa njia ya kuwaadhibu watu hao ni kuwaua, hivyo basi kitendo cha kuwaua siyo suluhisho sahihi kama alivyotanya Jalia kumuua Nungunungu kwa kosa la ubugumu uchumi, kwani Nungunungu alitakiwa kufungulwa kwa Mahakamani, Hivyo basi mwisho huo haujakidhi Matarajio ya jamii.

Pia, Mwandishi hajaonesha hatima ya Maandamano yaliyokuwa yakifanywa na Morani dhidi ya Ubugumu Uchumi, Maandamano hayo yaliyoongozwa na Jalia hayakuonekana hatima yake kwani kitabu kimeishia ta Dengo akiwa jukwaani akitaka kuyatajamajina ya wahujumu uchumi wa nchi na kabla hajayataja alipigwa risasi na kuuliwa. Hivyo huu mwisho si mzuri na hukutarajiwa na jamii kwani Mwandishi alitakiwa aonesha ni jinsi gani Watu hao wataka otajwa watakavyo chukuliwa hatua.

Kwa kufuatiwa na tamthiliya ya NGUZO MAMA, jinsi mwisho kivyokidhi Matarajio ya jamii?



7. Mwandishi hajaonesha njia sahihi ambazo
Zilitakiwa Zitumike Ili kuinua nguzo Mama; Mwisho
ni mwa tamthiliyo hivo tunaonesha tu kuwa
nguzo Mama haikuinuka ilibaki tu kuwa imelala
chini, hivyo basi wanajamii hawakutarajia kupata
Mwisho kama huo bali ilibidi mwandishi atoe
Mbinu gani Zitumike kuinua nguzo Mama na kitabu
kingesema kuwa nguzo Mama imeinuka, na siyo
kuwa chini.

Mwandishi hajatoa sababisho sahihi
la suala la unyanyasaji wa Mwanamke; Pia
tunaona kuwa Mwisho wa tamthiliya hii hakuna
mbinu yoyote iliyotolewa ambayo inawza kukome
sha suala zima la unyanyasaji wa Mwanamke,
kwani tunaonesha Bi piti alivyokuwa akinyanyasiwa
na Mumewe Sudi kwa kutanyishwa kazi nyingi
Pia kuchukuliwa pesa zake alizokuwa akizipata baada
ya kuuza pombe, hatima ya unyanyasaji huu haiku
onekana mwishoni mwa kitabu.

Pia; Mwandishi hajaonesha hatima ya
Unyanyasaji wa wajane baada ya kufiwa na waume
zao, hadi kufikia mwisho wa tamthiliya hii
tunaona kuwa Bi Saba baada ya kufiwa na Mumewe
alipokonywa mali zote ambazo zilikuwa zake na
Mumewe, B na Mwandishi hakuonesha hatua yoyote
iliyochukuliwa. Hivyo basi haya si matarajio ya
Mwandishi kwani mwisho wa kitabu ulitakiwa
uonishe hatua gani wanatakiwa kuchukuliwa watu
wanaowanyanyasa wajane.

Hivyo basi, Ili tamthilia ikidhi
Matarajio ya jamii inatakiwa kuishia kwa kutoa
Masuluhisho ama mbinu zinazotakiwa zitumike ili
kuondoa matatizo yanayoikumba jamii.

Kielelezo 7.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi jinsi miisho ya tamthiliya isivyokidhi matarajio ya jamii kwa kutumia tamthiliya ya “Morani” na “Nguzo Mama.”

Hata hivyo, asilimia 42.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11 kutokana na kutokuwa na maarifa toshelevu kuhusu miisho ya tamthiliya teule katika kukidhi au kutokidhi matarajio ya jamii. Kwa mfano, mtahiniwa

mmoja alitoa jibu lisilo sahihi kwa kutumia tamthiliya ya “Kivuli Kinaishi” ambayo kwa ujumla imekidhi matarajio ya jamii kwa kuwa mwandishi alitoa suluhisho la uongozi mbaya kwa kuangushwa kwa utawala wa Bi Kirembwe katika jamii ya Giningi. na hivyo kutokidhi matakwa ya swali hili. Hata hivyo, mtahiniwa huyo alitumia tamthiliya ya “Morani” na kutoa hoja zisizojitosheleza na kupata alama za wastani. Kielelezo 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyojitosheleza.

Kielelezo 7.2



7. Tamthilia ni sitori nchepu ya kuwasimua-
na zenye ujumbe katika jamii ~~na~~ unka tamthilia kuje-
nga mawazo yanayo enda kusaida jamii kwa ujumla
na kuendeleza kutatuma taz(iz) mbali mbali yanayo
zikumba jamii kwa ujumla.
Tamthilia zina undwa katika mjumbo tofauti
tofauti pia tamthilia ina weza kusaho na bila ku
to suluhisho katika jamii kwa kutumia vitabu
vinli tofauti. Nya tamthilia tamyosha ni ginoi-
gani tamthilia zinashindwa kuonesha ufisir na
kuto kazi mantegi ya jamii kwa kutumia ta-
mthilia ya KIVULI KINAISHI NA MORAN kwa-
kuanza na kitabu cha Kivuli Kinaishi kilichi
andikwa Said mohamed.
Kutaonesha suluhisho katika migogoro
ilyopo kwenye jamii katika kitabu cha Kivuli
kinaishi mwandishi ameshindwa kuonesha ni
nyisi gani ya kushinda mfuatana ilyopo ka-
tika Jamii kii enapeleka kutopata suluhisho
katika jamii unka mjano katiya mtoewa na
Bi Kirembwe kukosekana kwa suluhisho lami-
uitano yao.
Kushindwa kuonesha njaa nzuri za kuji
kombora katika nyanda mbali mbali za kuchum
katika tamthilia ya Kivuli Kinaishi msani ame
onesha kuwa kuwepo kwa watu wenye elimu sipo
nyia lais ya kujikwamua kuchum mo mfsamiali
pwisiwa kuonesha jamii wate madakitari na walimu
wazi kwa muewe sipi
Kushindwa kutoa maana anlimi ya kitabu
hii ni sababu nyingine inayo peleka wanafunzi wa
wa utabu kushindwa kujikosha ujumbe ulio kusudiwa



Kielelezo 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja zisizojitosheleza kwa kutumia tamthiliya moja sahihi. Aidha, mtahiniwa huyo alitumia neno la kiingereza ‘story’ na kuliandika ‘sitori’ isivyo halali.

Aidha, asilimia 17.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 6.5. Hii inatokana na kutoelewa matakwa ya swali na hivyo kujadili dhamira mbalimbali, migogoro au ujumbe ulio katika tamthiliya teule badala ya kueleza ni kwa jinsi gani miisho ya tamthiliya hizo isivyokidhi matarajio ya jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea dhamira mbalimbali zilizojitokeza katika tamthiliya ya “Morani” kama vile *kukithiri tatizo la uhujumu uchumi, kukithiri kwa ukosefu wa haki na kukithiri kwa suala la unyanyasaji wa kijinsia* na katika

tamthiliya ya “Kivuli Kinaishi” alitoa hoja kama vile; *kukithiri kwa uongozi mbaya, kukithiri kwa rushwa na kukithiri kwa ukoloni mamboleo.* Kwa ujumla, majibu hayo yalikuwa kinyume kabisa na matakwa ya swali, ikiwa ni pamoja na kutoa utangulizi na hitimisho lisiloendana na swali. Kielelezo 7.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili.

Kielelezo 7.3

7 Kwa kutumia tamthilia ya morani iliyoandikwa
na Emmanueli Mbogo na tamthilia ya nguzo mam
a iliyoandikwa na mwandishi Penina Muando
kwa kuanza na tamthilia ya Nguzo mama tuna
ona namna miisho ya tamthiliya isivyokidhi ma
tarajio ya jamii na hii ni katika suala la migogoro
Mgogoro kati ya Bi pili na mumewe bwana sudi;
chanzo cha mgogoro huu ni bwana sudi kutaka
kuchukua pesa za mkewe pili alizopata baada
ya kuuza pombe. suluhisho la mgogoro huu ni
bwana sudi kumpiga mkewe baada ya kukosa pesa
Mgogoro kati ya Bi-saba na Shemeji zake; Chanzo
cha mgogoro huu ni baada ya mume wa Bi-saba kufari
ki shemeji zake walikuja na kumchukua Bisaba
zile mali alizoridhi kutoka kwa mumewe suluhisho
la mgogoro huu ni Bisaba kuondoka katika eneo
lile. Hivyo tunaona kuwa miisho ya tamthiliya isivyo
kidhi matarajio ya jamii
Mgogoro kati ya sudi na wahokuwa wakimtetea
Bi pili asipigwe; mgogoro huu tunaona kuwa chanzo
chake ni bwana sudi kutaka kuchukua pesa za
mkewe na muisho baada ya kushindwa alichukua
hatua ya kumpiga mkewe suluhisho la mgogoro huu
ni rafiki zake bwana sudi kuambulia matusi
Kwa kutumia tamthilia ya ~~Nguzo~~ Morani tuna
ona namna miisho yake isivyokidhi matarajio ya
jamii kwa hoja zifuata zo
Mgogoro kati ya Jalia yusufu na mlemeta; Chanzo
cha mgogoro huu tunaona ni unafiki na uzembe
wa kazi kwa yusufu na Mlemeta walikua viongozi
wanafiki kitendo ambacho kilimchukiza Jalia katika
hili suala mgogoro tunaona sio matarajio ya jamii kusikia
vitu kama hivyo.

Kielelezo 7.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejadili migogoro mbalimbali iliyojitokeza katika tamthiliya ya “Nguzo Mama” na “Morani” badala ya kuelezea miisho ya tamthiliya hizo isivyokidhi matarajio ya jamii.

3.5.2 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* na lilihusu uhakiki wa vitabu teule vya tamthiliya na lilimtaka mtahiniwa kuchambua mandhari ya namna mbili kwa kila kitabu kuonesha jinsi yalivyosaidia kuibua maudhui kutoka katika tamthiliya mbili alizosoma. Swali lililenga kupima uchambuzi na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilikuwa la kuchagua na lilijibiwa na watahiniwa wengi zaidi (82.5%) ikilinganishwa na swali lingine katika sehemu hii. Swali hili lilijibiwa vizuri sana ambapo asilimia 97.0 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 12 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.



Chati Na. 12: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Kati ya watahiniwa wote waliojibu swali hili, asilimia 81.4 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 19. Miongoni mwao, asilimia 14.1 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kwa kuwa waliweza kuchambua mandhari ya namna mbili katika tamthiliya teule na kuonesha jinsi yalivyosaidia kuibua maudhui katika tamthiliya hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuchambua mandhari kwa usahihi katika tamthiliya ya "Morani" kama vile; mandhari ya msituni iliyoibua maudhui ya *umoja na mshikamano*; na mandhari ya ofisini iliyoibua maudhui ya *kupinga uhujumu uchumi* na *kujitoa mhanga* katika mapambano. Katika tamthiliya ya "Nguzo Mama" alichambua mandhari ya nyumbani iliyoibua maudhui ya *unyanyasaji wa mwanamke, mila potofu na suala la malezi bora kwa familia*; mandhari ya kilabuni iliibua maudhui ya *ulevi, kutokuwajibika na uvivu kunakosabishia jamii kuwa maskini*. Kielelezo 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vizuri na kupata alama za juu.

Kielelezo 8.1

8. Mandhari ni mahali au sehemu ambapo tukio la kifasihi hutendeka. Mandhari yanaweza kuwa jukwaani, ponni, uwanjani; ofisini na sehemu mbalimbali hata mapangoni. Mandhari imegawanyika katika sehemu mbili ambapo kuna mandhari ya kweli na mandhari ya kubuni; zote hutumiwa na waandishi ili kutimiza lengo la kazi ya fasihi. Pia mandhari husaidia kuibua maudhui katika kazi ya fasihi. Kwa kutumia tamthiliya mbili ambazo ni MURANI iliyoandikwa na EMMANUEL MBOGO na tamthiliya ya NGUZO MAMA iliyoandikwa na PENINA MUHANDO. Ifuatavyo ni jinsi mandhari yaliyosaidia kuibua maudhui; ~~kuto~~ kwa kuanza na tamthiliya ya MURANI ni kama ifuatavyo -

Mandhari ya msituni; hii ni mandhari iliyotumiwa na mwandishi kuibua suala la mgogoro ambapo tunaona Mzee; Mapoto na Malongo walikuwa wakibishana kuhusu dongo wakati walipokuwa njiani kuelekea kutafuta nguzo ya uswezi

Pia mandhari hii imeibua suala la umoja na mshikamano ambapo; watu hawa watatu walishikamana bila kukata tamaa ili kutafuta haki ili iweze kupatikana kupitia nguzo ya uswezi.

Mandhari ya ofisini; hii pia ni moja ya mandhari zilizojitokeza katika tamthiliya hii ambapo tunapata mandhari ya ofisini kwa Dongo ambapo ~~suala~~ imeibua suala la kupinga uhujumu uchumi. Dongo alikuwa kiongozi wa kamati ya kupinga na kwandaa listi ya majina ya wahujumu uchumi kwa hiyo kazi hiyo ilifanyika ofisini kwake pale alipokuwa akimwambia waandike majina ya wahujumu uchumi.

8 Mandhari hii ya ofisini pia imesaidia kuibua suala la mgogoro kati ya Jalia na Yusufu na Mlemeta ; mgogoro huu uhibuka baada ya Yusufu na Mlemeta kutoliandika jina la Nungu nungu ambaye ni mhujumu uchumi mkubwa. Kutokana na hali hii ikapelekea kutokuelewana kwa wafanyakazi hawa. Hivyo basi mwandishi ametumia mandhari ya ofisini kuibua maudhui katika kazi yake ya kifasihi

Pia kwa kutumia tamthiliya ya NGUZO MAMA ; zifuatazo ni mandhari na jinsi zilivyosaidia kuibua maudhui ;-

Mandhari ya nyumbani. ~~kwa~~ Bi ~~pili~~ ; mandhari hii imesaidia kuibua maudhui mbalimbali katika tamthiliya hii. Mfano ; nyumbani kwa Bi saba kuliibuka na suala la unyanyasaji wa mwanamke na mila potofu ambapo tunaona bi saba ananyanganywa na kuporwa kila kitu alichonacho pamoja na watoto baada ya mume wake kufariki, shemeji zake ndio waliomtendea hivyo.

Pia mandhari hii imesaidia kuibua suala la malezi bora ; mandhari ya nyumbani pia imetumika na kusaidia kuonesha suala la malezi bora kwa familia ambapo tunaona nyumbani kwa Bi pili jinsi mwanamke huyu anavyojitahidi kutunza familia yake vizuri kwa kufanya kazi kwa bidii.

Mandhari ya kilabuni. Katika mandhari hii imesaidia kuibua suala la mgogoro uliotokea kati ya bi pili na mume wake bwana sudi. Mgogoro huu ulitokea baada ya bwana sudi kutaka pesa kutoka kwa mke wake kwa lazima ;



8. baada ya mke wake kukatwa kumpatia pesa akamza
kumpiga. Hii inakwamisha maendeleo ya familia
na jamii pia kwani pesa zinatapotwa ili kuleta
maendeleo lakini sababu ya ulevi na kutojitambua
kunapelekea kukwamisha maendeleo kama tuyotikea
kwa bipili.

Imesaidia kutoa ujumbe kwa jamii kwa
jamii iachane na suala la ulevi na kuanza
kupeniya kazi kwa bidii ili kujenga jamii mpya
yenye maendeleo. Huyo katokana na mandhari
hii ya Kitabuni mwandishi anataka jamii
kubadilika ili kuleta mabadiliko katika jamii.

Kwa ujumla ; matumizi ya mandhari yanasaida
kuibua maudhui katika kazi ya fasihi kama vile
kutoa ujumbe kwa jamii hivyo; kuonyesha
matatizo mbalimbali yanayotokea katika jamii kama
vile ulevi, unyanyasaji na uongozi mbaya lakini
pia hutumiwa ili kuibua na kutatua migogoro
katika jamii.

Kielelezo 8.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyechambua kwa usahihi mandhari ya namna mbili kwa kila kitabu na kuonesha jinsi yalivyosaidia kuibua maudhui katika tamthiliya ya "Morani" na "Nguzo Mama."

Asilimia 15.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya hoja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichambua mandhari nne kwa kila kitabu na kueleza maudhui mbili zililizoibuliwa kwa kila mandhari kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutokukidhi matakwa ya swali.

Kielelezo 8.2

8 Mandhari ni mahali na muda wa utendekaji wa kazi ya fasihi, kuna mandhari ya namna mbili ambazo ni mandhari halisi na mandhari ya kubuni, Mandhari halisi ni aina ya Mandhari ambayo huwawili mazingira halisi ya jamii kama vile Shuleni wakati mandhari ya kubuni ni aina ya mandhari ambayo ~~ko~~ ni ya kufikirika tu hakuna aliyewahi kuiona kama vile kuzimu na mbinguni, kwa kutumia Tamthiliya ya "MOBANI" ~~na~~ iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo pamoja na tamthiliya ya "- "KIVULI KINAISHI" iliyoandikwa na Said Mohamed wwaandishi wametumia mandhari mbalimbali ili kuibua maudhui kwa kuanza na tamthiliya ya "MOBANI" Zifuatazo ni mandhari zilizojitokeza na kuibua maudhui kama ifuatavyo:-

Mandhari ya nyumbani kwa Nungunungu, mandhari hii inaibua mgogoro kati ya Jalia na Nungunungu baada ya Jalia kwenda nyumbani kwa Nungunungu kwa lengo la kumkamata unatokea mgogoro baada ya Nungunungu - kugwaamisha askari wake wamtoe nje Jalia.

Mandhari ya baa, hii ni mandhari ambayo - inaibua duala la ulevi, Mwandishi anamuonesha Aisha na Yusufu wakiwa baa wakihudumiwa pombe mbalimbali na Okashi.

Mandhari ya Ofisini, hii ni mandhari ambayo -- imetumika kuibua dhamira ya usaliti, baada ya Mlemeta na Yusuph kupewa hongo na Nungunungu ili wamuweke katika Orodha ya wahujumu Uchumi Yusufu na Mlemeta walimsaliti Jalia ambaye walikuwa katika kamati moja ya kuandaa orodha ya wahujumu uchumi baada ya kupewa hongo inapelekea Yusuph na Mlemeta kuwa wafuasi wa Nungunungu.



8 Mandhari ya jukwaani, mandhari hii imetumika kuonesha Unyonyaji unaofanywa na watu wenye madaraka, jukwaa hili lilandaliwa na Jalia na wenzake kwaajili ya kuibua wahyumu uchumi lakini longo lao halikufanikiwa kwani Longo alipigwa risasi na kufa pale jukwaani.

Vikuvile katika tamthiliya ya "kivuli kinaishi" kuna - mandhari mbalimbali zilizojitokeza ambazo zimeibua Maudhui kama ifuatavyo

Mandhari ya Giningi, hii ni mandhari kuu ya tamthiliya hii ambayo inazungumzia mambo mbalimbali yanayofanywa na Serikali kwa wananchi wake nchi hii ya Giningi ni Maskini kutokana Unyonyaji, rushwa na matabaka.

Mandhari ya Nyumbani kwa Bi ~~Mtokwa~~ kilembwe, huyu ni kiongozi mkubwa katika nchi ambaye ~~ana~~ anapenda rushwa na Unyonyaji nyumbani kwake kuna wali ambao amewanyweshwa Unga wa ndege unaowafanya wasijitambua hivyo mandhari hii - inaibua dhamira ya Ujinga.

Mandhari ya Shambani, hii inaibua dhamira ya - rushwa baada ya bawaba kumnyang'anya mkulima mzazo ambayo amelima kwaajili ya familia yake.

Mandhari ya getini, hii inaibua ~~dhami~~ Ujumbe wa kujitambua ambaye anaelekea nyumbani kwa Bi - ~~Mtokwa~~ kilembwe kwaajili ya kupambana nae kwa - kuwalisha watu unga wa rutuba (maarifa) kwaajili ya kuikomboa jamii yake.

Kielelezo 8.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa yasiyojitosheleza kutokana na kushindwa kuzingatia matakwa ya swali ipasavyo.

Watahiniwa wachache sana (3.0%) pekee ndio waliofanya swali hili na kupata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6 kutokana na kushindwa kuchambua mandhari ya namna mbili na kuonesha jinsi yalivyosaidia kuibua maudhui katika tamthiliya mbili teule. Mapungufu makubwa ya watahiniwa hao ni pamoja na kutaja mandhari bila kuonesha maudhui zilizoibuliwa, kutoa hoja pungufu au kutoa maelezo mafupi sana yasiyotosheleza matakwa ya swali pamoja na kutozingatia taratibu za uandishi wa insha ipasavyo.

Kielelezo 8.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekosa maarifa katika kujibu swali hili ipasavyo licha ya kuchambua baadhi ya mandhari zilizo sahihi.

Kielelezo 8.3



8. Tamthiliya
Nguzo Mama iliyo andikwa na Penina Mhando
Mandhari
Kijijini na Mandhari ya Mjini

Mandhari ya kijijini
Wamama wapo wanashirikiana ni namna gani watainua nguzo mama ikapelekea dhamira ya ~~kazi~~ Umoja na ushirikiano.

Mandhari ya mjini
Mume wa bi sita yupo na gari na wanawake pia muda mwingine alikuwa na bi tano (huko mjini. Ambapo mandhari hiyo ilipelekea dhamira ya Usahti.

Tamthiliya kivuli kinaushi - Said Mohamed.
Mandhari ya kijijini ~~na ya Mjini~~ ambapo mandhari ya kijijini wali amini ya kuwa kivuli kinaishi kama jinsi ambavyo wahitumia baadhi ya imani mbalimbali kama vile Giningi, unga wa Ndere, ambao ulipelekea dhamira ya Imani potofu, na kisingozi was alikuwa bi. Kirembwe.

Kielelezo 8.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuandika majibu kwa muundo wa insha kama ilivyotakiwa badala yake akaandika kwa njia ya *dondoo* bila maelezo ya kutosheleza na kupata alama za chini.

3.6 SEHEMU E: USANIFU WA MAANDISHI

3.6.1 Swali la 9: Usanifu wa Maandishi

Swali lilitoka katika mada ya *Usanifu wa Maandishi* na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20 na lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari na kisha kujadili mbinu za kifani zilizotumika kufikisha ujumbe.

Swali hili lilikuwa la lazima ambapo watahiniwa wote waliofanya mtihani walilijibu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi kwani asilimia 90.5 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 13 inaonesha viwango vya watahiniwa vya kufaulu kwa asilimia.



Na. 13: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Takwimu zinaonesha kuwa, kundi kubwa la watahiniwa (64.3%) waliofaulu katika swali hili ni wale wenye kiwango cha wastani ambao walipata alama kuanzia 7 hadi 11.5. Watahiniwa hao walieleza baadhi ya mbinu anuai za kifani zilizotumika katika matini kwa usahihi na kushindwa kubaini mbinu nyingine za kisanaa. Pia kulikuwa na baadhi ya watahiniwa waliojadili mbinu za kifani zilizotumika kufikisha ujumbe katika kifungu cha habari kama; *muundo, mtindo, wahusika na mandhari* kwa usahihi lakini wakashindwa kubaini matumizi ya lugha kwa baadhi ya vipengele. Kwa ujumla, watahiniwa hao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tamathali za semi kwani wengine walibaini mbinu hizo kinyume na zilivyotumika katika kifungu cha habari kama vile; *pilipili usiyoila*... (tashbiha) badala ya kubainisha kama methali.

Aidha, asilimia 16.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri na kupata alama kuanzia 12 hadi 19. Hii

inatokana na sababu kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya kusanifu maandishi katika matini za kifasihi na hivyo kujadili kwa usahihi mbinu za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari walichopewa. Pia, watahiniwa hao waliweza kueleza mbinu za kifani zilizotumika katika habari waliyopewa kwa usahihi kama vile; mtindo, muundo, matumizi ya lugha (tamathali za semi, misemo, methali na nahau) wahusika na mandhari. Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeelezea mbinu mbalimbali za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari kama ilivyotakiwa.

Kielelezo 9.1

9. i/ Aina ya matini – ni hadithi au riwaya inayoelezea kisa cha Yasmin na mwajuma kuanzia walipoanza kurushiana maneno hadi kupigana na kununiana siku tatu.

ii/ Muundo – Ni mtiririko wa visa katika kazi ya fasihi.
– Muundo wa hadithi hii ni wa moja kwa moja ambao umegawanyika katika aya saba zinazoelezea ugomvi wa mwajuma na Yasmin.

iii/ Mtindo – Ni ufundi wa kisanaa anautumia mwandishi katika kupanga kazi yake.
– Mtindo wa masimulizi ambapo msimuliaji anasimulia hadithi ya kisa cha Yasmin na Mwajuma. Matumizi ya funga na fungua semi.
– Mtindo wa nafsi, nafsi zote tatu zimetumika. Mfano: nafsi II umoja – Na weye nawe na Denge wako, kila uambialwo. nafsi ya I umoja Mimi?

iv/ Wahusika – Ni watu au vitu vinavyotumika katika kazi ya fasihi.
– Mwajuma, rafiki wa Yasmin ambaye aligombana na rafiki yake hadi kupigana.
– Yasmin, rafiki wa mwajuma aliyegombana nae na kununiana siku tatu bila kuongea.
– Majirani, waliwaamulia Yasmin na mwajuma ugomvi wao.

v/ Mandhari – Ni sehemu ambayo kazi ya fasihi hute ndeka huweza kuwa halisi au ya kubuni.
– Mandhari ya chumbani kwa mwajuma na Yasmin ambapo ugomvi ulitokea.

vi/ Matumizi ya Lugha – Ni jinsi msanii anavyotumia Lugha katika kazi yake ya



9. Matumizi ya Lugha - Kifasihi. Matumizi ya Lugha huwa ni methali, nahau, mafumbo na tamathali za semi.
- Nahau, hana mbele wala nyuma
- Methali, pilipili usiyoila-----
- Tamathali za semi
Mdokezo, n'na mume wangu yuko----
Tashbiha, anapiga mikambi kama chatu
Tashihis, midomo haina breki.
- Lugha ya kutohoa, breki
- Matumizi ya Lahaja, "Na weye nawe na Denge wako, (Kiunguja)
Lahaja ya Kihindi, "Mwenye laana weya kahaba mkubwa"
- Tashbiha, amenasa kama nzi aliyenasa na uzi wa buibui.
- Tanakari sauti, puuu!

Kielelezo 9.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kutokana na kujadili kwa usahihi mbinu za kifani katika kifungu cha habari.

Licha ya swali hili kufanyika vizuri, watahiniwa wachache asilimia 19.5 walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama za chini kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kushindwa kujadili mbinu anuai za kifani zilizotumika kufikisha ujumbe katika kifungu cha habari walichopewa. Baadhi ya watahiniwa walijadili vipengele vya maudhui kama vile *dhamira, migogoro, ujumbe, falsafa na msimamo wa mwandishi* kinyume na matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa wengine walibadili methali *pilipili usiyoila....* kuwa ni kitendawili na kubaini aina ya misemo ambayo haikutumika katika kifungu cha habari. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza mbinu za kifani kama, *tafsida, tashbiha na tamathali za semi* lakini maelezo yake yalikuwa kinyume na uhalisia wa matumizi ya vipengele hivyo katika matini aliyopewa. Pia mtahiniwa huyo alitaja mtindo uliotumika katika kifungu cha habari kuwa ni *mtindo wa lugha* na kujadili *falsafa* kama mbinu ya kifani kinyume kabisa na mbinu anuai za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa

kujadili mbinu za kifani zilizotumika kufikisha ujumbe kutoka katika kifungu cha habari.

Kielelezo 9.2

9. ii/ Tafsida
- kuna matumizi ya lugha ya uficho yaliyojit
okeza kwenye kifungu cha habari.
Mfano; Pilipili usiyoila....."

9 iii/ Tashbiha
- Pia kuna Mbinu nyingine ya kifani iliyojito
keza kwenye kifungu cha habari ili iweze k
ufikisha ujumbe kwenye jamii.
Mfano; "Hee! mbona hivyo, umenishikilia kaolewe, kaolewe,
Mimi mke wa mtu hivyo, n'na mume wangu yuko
.....!

iii/ Tamathali za semi
- Vile vile kuna tamathali za semi kwenye kifungu
cha habari hii.
Mfano, "Nani kahaba? Mimi? Usokuwa na fadhila we
mjaa ...."

iv/ Mtindo wa lugha
- Pia mtindo wa lugha uliyotumika kwenye kua
ndika kifungu cha habari hii ni wa kuel
eweka ambao umetumia matamshi mepesi.

v/ Falsafa
- vilevile kuwepo kwa falsafa ni kuwepo kwa i-
mani ya mwandishi. Mwandishi anaamini kuwa
kupita kazi yake aliyoandika ili kufikisha uj
umbe kwa hadhira anaimani kuwa jamii
itaelimika kupitia kazi yake.

Kielelezo 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejadili *falsafa* na *mtindo wa lugha* kama mbinu za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari kinyume na matakwa ya swali.

4.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

Uchambuzi wa takwimu za kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili unaonesha kuwa, watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri katika mada kumi (10) kati ya mada kumi na moja (11) zilizotahiniwa ambapo ni mada moja (1) pekee iliyokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu.

Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na kile cha mwaka 2017 kimeongezeka katika mada nyingi kama ifuatavyo: *Riwaya* (99.4%), *Ushairi* (99.1%), *Maendeleo ya Kiswahili* (92.0%), *Usanifu wa Maandishi* (90.5%), *Tamthiliya* (89.8%), *Tafsiri na Ukalimani* (87.2%) na *Fasihi kwa Ujumla* (66.5%). Kwa mwaka 2017, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada hizo kilikuwa ni cha chini ambapo *Riwaya* (96.3%), *Ushairi* (98.7%), *Maendeleo ya Kiswahili* (82.6%), *Usanifu wa Maandishi* (87.2%), *Tamthiliya* (78.0%), *Tafsiri na Ukalimani* (42.2%) na *Fasihi kwa Ujumla* (36.3%). Hata hivyo, kumekuwa na ongezeko la kufaulu kwa mada za *Tafsiri na Ukalimani* (45.0%) na *Fasihi kwa Ujumla* (30.2%) kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na kiwango kidogo cha kufaulu kwa mwaka 2017.

Aidha, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2018 kimepungua katika mada ya *Utungaji* (98.7%), *Ufahamu na Ufupisho* (93.4%), *Sarufi* (68.4%) na *Utumizi wa Lugha* (52.9%) ikilinganishwa na mwaka 2017 ambapo kiwango cha kufaulu kwa mada hizo kilikuwa, *Utungaji* (98.9%), *Ufahamu na Ufupisho* (96.1%), *Sarufi* (68.7%) na *Utumizi wa Lugha* (72.2%), zilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha kufaulu ikilinganishwa na mwaka 2018. Ijapokuwa mwachano wa mada hizi kati ya mwa 2017 na 2018 kwa ujumla ni mdogo, mada ya *Utumizi wa Lugha* imekuwa na mwachano mkubwa zaidi kwani kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2018 kimeshuka kwa asilimia 19.3 ukilinganisha na kile cha mwaka 2017.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada karibu zote kwa mwaka 2018 kilikuwa kizuri isipokuwa mada ya *Utumizi wa Lugha* pekee iliyokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu. Hivyo, asilimia 85.3 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 35 katika mada zote. Kiwango hiki ni cha juu zaidi ikilinganishwa na kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kwa mwaka 2017 ambapo asilimia 79.8 walipata alama zaidi ya 35. Ongezeko hili (5.5%) la kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada kwa mwaka 2018 linaonesha kuwa, watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa.

5.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2018 kilikuwa kizuri ambapo asilimia **99.97** ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata alama 35 au zaidi. Kiwango kizuri cha kufaulu kimetokana na watahiniwa kuwa na ujuzi na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa. Kiwango hiki cha kufaulu kwa watahiniwa kimekuwa na ongezeko la asilimia **0.09** ikilinganishwa na kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2017 ambapo wastani wa kiwango cha kufaulu kilikuwa **99.88.**

Uchambuzi uliofanyika unaonesha changamoto mbalimbali za watahiniwa wachache walioshindwa kufanya vizuri kama vile; uelewa mdogo wa matakwa ya swali, mtiririko usiokidhi vigezo vya uandishi, uelewa mdogo wa mada mbalimbali na uwezo mdogo katika kujibu maswali. Kadhalika, watahiniwa hao walishindwa kutoa mifano sahihi na ya kutosha katika kujenga hoja za kujibu swali na kutokufuata maelekezo ya swali.

Mwisho, taarifa hii iwe changamoto katika kuwasaidia walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa yanayosababisha watahiniwa wachache kutokujibu vizuri maswali hususani katika mada ya *Utumizi wa Lugha*. Aidha, taarifa hii itakuwa na tija kwa walimu katika ufundishaji, utungaji na usahihishaji wa mitihani, na hivyo kuinua kiwango zaidi cha kufaulu kwa watahiniwa katika somo hili. Pia, taarifa hii italeta msukumo wa kujifunza kwa wanafunzi na hasa ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha inayotambulika na kutumika kitaifa na kimataifa ambapo kila mtahiniwa anapaswa awe na uwezo wa kujieleza vizuri, kujiamini na kujivunia lugha hii kama sehemu ya utamaduni wa mtanzania.

6.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi inapendekezwa kuwa:

(a) Mada ya *Utumizi wa Lugha*, iliyokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu, inasisitizwa kuwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa mada hiyo mbinu shirikishi itumike ikiwa ni pamoja na .

   (i) Ufundishaji na ujifunzaji wa mada ndogo ndogo za jinsi ya kutumia lugha zinatakiwa zipewe kipaumbele ili kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa mahsusi katika mada mbalimbali za *Matumizi ya Lugha*.

(ii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kutosha katika kutumia lugha ili kubaini kwa urahisi umuhimu wa mambo mbalimbali ya kuzingatiwa katika kutumia lugha.

(iii) Wanafunzi waaswe kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha ili kuwawezesha kung'amua umuhimu wa uhusiano wa wahusika wakati wa kutumia lugha.

(b) Serikali itoe vitabu vya kiada na ziada kwa somo la Kiswahili ili kuwa na usawa katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili na kuwa na rejea zinazofanana katika somo la Kiswahili.

(c) Walimu pamoja na wadau mbalimbali wa elimu kuendelea kuwatilia mkazo wanafunzi katika kujifunza mada ya *Matumizi ya Lugha* ili kuinua kiwango cha kufaulu katika mada hiyo.

Kiambatisho A

ULINGANIFU WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2017 na 2018

Na.	Mada	2017			2018		
		Idadi ya Maswali	Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Asilimia 35 au Zaidi	Maoni	Idadi ya Maswali	Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Asilimia 35 au Zaidi	Maoni
1.	*Riwaya*	2	96.3	Vizuri	2	99.4	Vizuri
2	*Ushairi*	2	98.7	Vizuri	2	99.1	Vizuri
3.	*Utungaji*	1	98.9	Vizuri	1	98.7	Vizuri
4.	*Ufahamu na Ufupisho*	2	96.1	Vizuri	2	93.4	Vizuri
5.	*Maendeleo ya Kiswahili*	2	82.6	Vizuri	2	92.0	Vizuri
6.	*Usanifu wa Maandishi*	2	81.9	Vizuri	2	90.5	Vizuri
7	*Tamthiliya*	2	78.0	Vizuri	2	89.8	Vizuri
8.	*Tafsiri na Ukalimani*	1	42.2	Wastani	1	87.2	Vizuri
9.	*Sarufi*	2	68.7	Vizuri	2	68.4	Vizuri
10.	*Fasihi kwa Ujumla*	2	36.3	Wastani	2	66.5	Vizuri
11.	*Utumizi wa Lugha*	2	72.2	Vizuri	2	52.9	Wastani

Kiambatisho B